# Nipashe

Jumanne Juni 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580983

www.ippmedia.com

MWANGA WA

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 70

LIKE & FOL



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 260,838,830

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#





**Ufaransa** yamwaga mabilioni mradi wa maji

UKURASA 4



**MARTINEZ BADO MUHIMU INTER MILAN**

UKURASA 22



Ujenzi ukiendelea katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MAKTABA**

# Mbunge 'aliamsha' bungeni

• **Amtaka** Spika kuunda tume huru kuchunguza miradi ya.... *Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MAHAKAMA YATOA SIKU 14 UPELELEZI KESI YA SABAYA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro imeutaka...

UKURASA WA 3

**LOTTERY CLUB YAIUNGA MKONO EATV NAMTHAMINI**

KLABU ya Lottery tawi la Oysterbay jana imekabidhi pedi 10,500 katika kituo cha...

UKURASA WA 7

**MWINYI AHAKIKISHIA WADAU MAZINGIRA RAFIKI**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi...

## Mtendaji matatani tuhuma kusababisha mauaji ya mtoto

UKURASA 3




Rais wa Rotary Club Oysterbay, Aisha Sykes (kulia), akikabidhi taulo za kike katoni 10,000 kwa Mwenyekiti wa IPP, Abdiel Mengi, zilizotolewa na klabu hiyo kwa ajili ya wasichana wanaosoma kupitia kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na East Africa Radio na EATV katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam jana. Wapili kulia ni Rais wa Rotary International, Shekhar Mehta, Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Television Ltd, Regina Mengi (wapili kushoto) na mama Rashi Mehte. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali yapingwa mikopo 10%

UK.2

**MICHEZO** SIMBA KUSAJILI FOWADI YA MABAO 47 UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Mwenyekiti wa Taasisi ya Fursa Sawa kwa Wote, Mama Anna Mkapa, katika maadhimisho ya miaka 25 ya taasisi hiyo jijini Dar es Salaam jana.(**Habari kamili Uk.7**) **PICHA: IKULU**

# Mbunge 'aliamsha' bungeni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Kisesa (CCM), Luaga Mpina, amemtaka Spika wa Bunge kuunda tume ya kuchunguza kusuasua ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, biashara ya mbolea, kupanda kwa bei ya mafuta kwa kisingizio cha vita ya Ukraine na Russia na ukusanyaji wa mapato.

Aidha, amepinga Waziri wa Fedha na Mipango, kupewa mamlaka ya kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na mapato kwa wawekezaji mahiri, huku akitaka usawa kwa wote.

Akichangia mjadala wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23, jana bungeni, alisema iwapo Spika atapokea ushauri wake atamshukuru baadaye kwa kuwa atakuwa amefanya jambo zuri kwa manufaa ya taifa.

"Mheshimiwa Spika nakuomba ukubali uweke hii rekodi utanishukuru, utakapounda tume ya bunge utakayoenda kuyaona na mchango utakaoleta kwenye taifa utanishukuru kama mmoja wa wabunge wako niliyeleta hoja hii," alisema.

Alitaka pia kuundwa tume ya kuchunguza sababu za kupanda kwa bei ya mafuta kwa kisingizio cha vita ya Ukraine na Urusi.

"Tuweze kujua makondokando yaliyomo humo ndani ya bei za mafuta, kupanda kwake nchini kuna nini kimejificha," alisema.

Mpina aliyewahi kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alitaka tume hiyo kuchunguza bei za mbolea nchini na biashara inavyofanyika kwa kuwa zamani nchi ilifanya vizuri zaidi kuliko sasa, ikiwamo kutembelea viwanda na kuwezesha mbolea kuagizwa kwa bei ndogo na kusambazwa kwa bei ndogo, utaratibu ambao kwa sasa haupo.

"Nataka nijue bei tunazopewa zina uhalisi, nataka iundiwe tume kwasababu hata Waziri wa Kilimo bungeni mchana alikuwa na takwimu nyingine na kuhitimisha akaja na takwimu nyingine, tutaka tujue ukweli na uhalisi wa mbolea wanazouziwa wananchi," alisisitiza.

Pia, alitaka tume kwenye malimbikizo ya kodi kwa kuwa yamefikia Sh. trilioni 7.54 zilizoshindwa kukusanywa huku uwezo ukiwa ni asilimia tano.

Aliitaka tume hiyo kupitia pingamizi ya kodi zilizoko na kwamba kuna kesi ya rufani za Sh. trilioni 5.19 zinatakwa kuamuliwa, lakini haziamuliwi na matokeo yake mapato ya serikali hayakusanywi.

Alisema nchi za Rwanda na Kenya zinakusanya asilimia 16 ya pato la taifa huku Tanzania ni wastani 11. 4, huku akibainisha malimbikizo ya madeni trilioni 7.54 ambayo yanaifanya serikali kupoteza mapato mengi.

Alibainisha kuwapo kampuni 504 za kimataifa ambazo uchambuzi wake wa kodi lazima uwe na watu wenye uwezo wa kuchambua na kwamba uwezo ni asilimia 1.2 jambo linalodhihirisha mapato mengi kupotea.

"Deni la serikali limeongezeka kwa Sh. trilioni 8.72 kwa mwaka mmoja wa fedha ikimaanisha kuwa wamekopa kuliko kilichoahidiwa bungeni, tuli 'service' (hudumia) kwa Sh. trilioni 7.2, tumekopa mkopo mkubwa kuliko kilichoahidiwa bungeni na kama walifanya hivyo kwa ridhaa ya nani aliruhusu," alihoji.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, kwa hesabu za kawaida tumekopa zaidi ya Sh. trilioni 15 wakati tunaeleza tumekopa Sh. trilioni 9.3 na kwamba ni muhimu serikali ikaeleza kwa usahihi ili kujua utofauti.

Pia aliwataka wabunge kutokubali kupitisha sheria inayompa mamlaka Waziri wa Fedha na Mipango, kutoa vivutio vya ziada kama kusamehe kodi ya VAT na ya mapato kwa wawekezaji mahiri.

"Lazima tujue tuna ushindani sawa, kuna watu wamewekeza viwandani nchini leo anakuja mtu unamsamehe, kama tunataka kusamehe tusamehe wote ili kuwe na usawa kwa wote," alisema na kuongeza:

"Naomba Waziri wa Fedha, sio leo atakuwa waziri wa kudumu watakuja wengine asikubali na kuingizwa kwenye mtego wa kutoa kodi kwa kundi la watu, nasi wabunge tusikubali kuruhusu su hii sheria ikapita humu.

"Hawa ni mahiri tunawasamehe wakati una wawekezaji wengine nchini, wasiposhindana kwa haki si watafunga viwanda kwa ajili ya huyo uliyempendelea, tukatae sheria hizo, muswada wa fedha utakapokuja lazima tusema hatutaki usipite," alisema.

# Serikali yapingwa punguzo 10% mikopo kundi maalum

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuacha mpango wa kupunguza asilimia 10 ya mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu badala yake itafute fedha sehemu nyingine za kujenga majengo ya machinga.

Pia, imetakiwa kufanya uchunguzi kabla ya utekelezaji.

Wakichangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23, wabunge hao walisema fedha hiyo ambayo inatokana na mapato ya halmashauri kuna maeneo hawaitoi kuwezesha makundi hayo kufikia malengo na ikipunguzwa itawaumiza wananchi pamoja na kutofikia lengo la kuongeza walipa kodi.

Asilimia 10 hutolewa kwenye mapato ya halmashauri ambayo hukopeshwa wajasiriamali wa halmashauri husika kwa mlingano wa asilimia nne wanawake, nne vijana na mbili wenye ulemavu.

Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Christina Ishengoma, alisema ni vizuri serikali ikaacha kupunguza asilimia 10 ya mikopo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu, na badala yake iziongeze na kujenga miundombinu ya machinga kwa fedha nyingine.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Shally Raymond, alisema asilimia 10, ilipowekwa ilikuwa na madhumuni maalum tangu mwaka 1994, na ilianza kwa kiwango hicho kwa wanawake wasiokopesheka wawezeshwe kuwa na biashara, kwa kuamini ukiwezesha kaya umewezesha taifa.

"Iweje leo serikali inataka kujenga miundombinu inakuja pale pale kwenye asilimia 10, mwaka juzi ilipunguzwa ikawa nne na sasa mmekuja mnataka kupunguza tena hali itakayoongeza mzigo kwa wananchi," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Tauhida Kasiani, alisema kuchukua asilima tano kwa ajili ya machinga haijakaa vizuri, ziachwe kwa ajili ya kusaidia makundi maalum.

"Ili likae vizuri machinga wanapatikana kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu hawajazuiwa kwenda kufanya kazi au kuomba mikopo, waziri pata muda fuatilia kama unafanya kazi vizuri," alisema na kuongeza:

"Kuna halmashauri zimelimbikiza miaka mingi hazijatoa mikopo, tukisema tunaondoa asilimia tano wakati hata zilizoko watendaji wameshindwa kuzitoa ni kuumiza wananchi, kwa sasa ni mapema mno na tumefanya haraka tusubiri kwanza."

Naye Mbunge wa Mvumi (CCM), Livingstone Lusinde, aliitaka serikali kufanya utafiti kujua mahitaji ya machinga, kwa kuwa huenda wanachotaka sio serikali inachofanya.

"Wanataka mahali penye mrundikano hawahitaji jengo zuri, unaweza kuwajengea na wasikae. Waziri wa Fedha alipokuwa anasema asilimia 10 kwenye Mpango wa Taifa lengo ni kuzalisha mabilionea wengi ni kwa utaratibu huu au kuna mwingine, maana unapataje mabilionea kwa utaratibu wa kuwaondolea asilimia tano?" Alihoji.

"Miundombinu, asilimia 10 inakwenda kwenye mitaji na machinga walikopa huku na sasa zinapunguzwa kwenda kujenga miundombinu, sasa wanasema asilimia tano zijenga miundombinu huku hujui wamachinga waliopo," alisema.

Kwa mujibu wa Lusinde, ni bora asilimia 10 ibaki na itafutwe nyingine ya kwenda kujenga miundombinu.

Naye, Mbunge wa Kisesa, Luaga Mpina, alisema serikali iangalie upya suala la asilimia 10 ya makundi hayo kwa kuwa mahitaji ya machinga yanatofautiana kutoka eneo moja hadi jingine.

Alisema ni muhimu kujiuliza kwamba machinga wa Meatu mahitaji yake ni sawa na ya yule wa eneo jingine, kwa kuwa sio wote wenye kuhitaji majengo, huku akitaka serikali kutafuta fedha kwingine ya kujenga miundombinu hiyo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kinondoni (CCM), Abas Tarimba, alisema sheria ya utawala wa kodi inatakiwa kufumuliwa, ili kutanua wigo wa walipa kodi na kwamba sio kuongeza viwango bali kwa kuweka vidogo ili wengi walipe.

Alisema misamaha ya kodi haitalisaidia taifa huku akitolea ya simu janja na taulo za kike ambalo ilisamehe na kusaidia wafanyabiashara.

Pia alisema kuna kodi zimepunguzwa kunufaisha wafanyabiashara na sio wananchi na kutoa mfano kodi ya mitungi ya gesi ambayo itamnufaisha mwenye kiwanda wakati serikali ilitakiwa kupunguza kodi kwenye gesi ili ishuke bei.

HABARI KITAIFA



Mabanti waliokimbia vitendo vya ukeketaji kutoka majumbani kwao, wakiwa katika mafunzo ya kushona nguo yanayotolewa na Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, jijini Dar es Salaam juzi, ili kupata ujuzi utakaowawezesha kuendesha maisha yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mahakama yatoa siku 14 upelelezi kesi ya Sabaya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro imeutaka upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi wa kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake wanne ili kila mshtakiwa apate haki kwa mujibu wa sheria.

Akitoa amri hiyo, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Salome Mshasha, aliwataka upande huo kuharakisha upelelezi ndani ya siku 14.

"Hoja za upande wa utetezi ni za msingi, nakala zinaonyesha mwanzoni mlipoleta kesi hii mahakamani hapa mlisema uchunguzi umekamilika," alisema Hakimu Mshasha.

Wakili wa Utetezi, Helena Mahuna, alidai upande wa utetezi haupo makini katika ufuatiliaji wa kesi hiyo kutokana na ucheleweshaji wa kukamilika kwa upelelezi.

"Mheshimiwa upande wa Jamhuri walipofika mahakamani hapa mara ya kwanza waliieleza mahakama yako tukufu kwamba upelelezi umekamilika na wanasubiri kibali cha hati itakayotoa kibali kwa mahakama hiyo kuanza kusikilizwa kwa kesi.

"Kesi hii iliporudi hapa upande huo huo wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika na leo ni mara ya pili wanakuja hapa na kusema upelelezi haujakamilika, hili halituridhishi kutokana na wateja wetu wanaendelea kuteseka gerezani bila kufahamu hatima yao ukizingatia bado mshtakiwa namba moja anaumwa sana," alidai Wakili Mahuna.

Wakili Mahuna alidai kuwa kuendelea kupigwa tarehe kesi hiyo ni kuwatesa washtakiwa hao na kuongeza kuwa mshtakiwa namba moja anaumwa sana.

Akiomba tarehe ya kutajwa, Wakili wa Serikali Mwanandamizi, VeredIana Mlenza, aliiomba mahakama siku ya kutajwa kesi hiyo.

"Upelelezi bado haujakamilika, tunaomba muda ili kuhakikisha tumepata kibali kutoka kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu ili kutoa kibali," alisema.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, kosa la kwanza katika kesi hiyo ambalo linawahusu washtakiwa wote ni la kuongoza na kushiriki genge la uhalifu katika Wilaya ya Hai, Februari 2, mwaka jana.

Shtaka la pili, linamkabili mshtakiwa wa kwanza, Lengai Ole Sabaya, ambalo anadaiwa kulifanya Februari 22, mwaka jana, kwa kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Katika shtaka la tatu, Ole Sabaya peke yake, anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai, kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

# Mtendaji mbaroni tuhuma za kusababisha mauaji ya mtoto

**Na Anjela Mhando,** SIHA

OFISA Mtendaji wa Kata ya Kirua, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Godson Munisi, ameingia matatani baada ya kudaiwa kuagiza kukamatwa, kupigwa na kuteswa mtoto Bright Arnold (anayekadiriwa kuwa na miaka saba - 10) na kupoteza maisha.

Tukio hilo, limesababisha familia ya marehemu kugoma kuuzika mwili hadi serikali itakapotoa tamko na kuchukua hatua.

Marehemu Bright, anadaiwa kushambuliwa kwa kipigo na askari wawili wa Jeshi la Akiba (Mgambo), Juni 16, mwaka huu, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, akituhumiwa kuiba ndala na yeboyebo za daktari mmoja wa binadamu katika Kijiji cha Fuka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Simon Maigwa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema mtendaji huyo kwa sasa anashikiliwa na Polisi kutokana na tuhuma za mauaji hayo.

"Ni kweli tunamshikilia Mtendaji (Munisi). Swali la kujiuliza, hata kama mtu ni mwizi, huwezi kuruhusu wananchi wajichukulie sheria mkononi. Tunamshikilia, lakini tunatafuta wengine walioshiriki," alisema ACP Maigwa.

Baadhi ya mashuhuda waliiambia Nipashe kuwa Bright kabla ya kupoteza maisha, alikimbizwa katika Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto kupatiwa matibabu, lakini hali yake ilizidi kuwa mbaya na baadaye kuhamishiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC na kufariki dunia akiwa chumba cha uangalizi maalum (ICU).

Baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo, wamelaani kitendo hicho wakitaka mamlaka za serikali kuwasaka na kuwakamata wote waliohusika na mauaji hayo.

Shuhuda wa tukio hilo, Julieth Mrang'u, mkazi wa Kijiji cha Fuka, aliiambia Nipashe kwamba alifika ofisi ya kata hiyo na kumkuta Bright akipigwa.

Kwa mujibu wa shuhuda huyo, wakati tukio la kipigo likiendelea, kaka wa marehemu alifika katika ofisi hizo na kukuta mdogo wake akiwa hoi kwa kipigo.

"Baada ya kaka yake kufika, Bright alimwomba kaka yake akamnunulie maji, kaka yake alipomnunulia alishindwa kunywa na kilichofuata mtoto akajisaidia hapo hapo na kuzimia.

"Kama mtoto alikuwa ni mwizi wangemkamata na kumpeleka katika kituo cha polisi ili sheria ichukue mkondo wake, lakini mtendaji na migambo waliamua kujichukulia sheria mkononi na kumpiga.

"Tunaomba serikali itusaidie juu ya suala hili, sisi hatuziki huyu mtoto, tunataka mtoto wetu."

Akizungumzia tukio hilo, mama wa marehemu, Ruth Munuo alisema: "Mimi sikuwapo nyumbani siku hiyo, nilikuwa nimetoka. Nilipewa taarifa kwamba mwanangu (Bright) amechukuliwa na mgambo wa kata.

"Nilipokwenda kumfuatilia huko ofisi ya kata, nikakuta mgambo wa kata na mtendaji wamejifungia ndani na mtoto. Halafu kulikuwa na watoto wengine pia, wakiwa wamekalishwa chini, wanapigwa maeneo mbalimbali ya kichwa, mikono na miguuni kwa kutumia rungu," alidai mama huyo.

Watoto wengine, wanaodaiwa kupigwa ni Stanley Maimu, Ernest Macha na mwingine aliyefahamika kwa jina moja la Rama.

Akieleza zaidi, mama huyo alisema: "Nikiwa pale, nilitaka kuongea naye, mtoto alikuwa ameshazimia, ameanguka na wengine wakawa wanasema anajidai kazimia. Ndiyo mtendaji akamchukua akampeleka hospitali na mtoto kufika kule hakuongea tena.

"Ninamwomba mbunge kwa kushirikiana na serikali itusaidie kuangalia jambo hili kwa sababu wananchi wanyonge wamekuwa wakinyanyaswa, mtoto huyu amekufa kifo cha mateso."

# Lottery Club yaiunga mkono EATV kampeni Namthamini

**Na Jenifer Gilla**

KLABU ya Lottery tawi la Oysterbay jana imekabidhi pedi 10,500 katika kituo cha East Afrika Televisheni na Radio ikiwa ni ushirikiano wa kampeni ya 'Namthamini' inayolenga kugawa pedi kwa wanafunzi kuwasaidia kuwa salama wanapokuwa kwenye hedhi.

Akiongea katika hafla ya kukabidhi taulo hizo, Rais wa klabu hiyo, Aisha Sykes, alisema wameguswa kushiriki kampeni hiyo ili kumaliza tatizo la watoto wa kike kutohudhuria masomo kwa sababu ya kupata hedhi.

Alisema mchango huo ni takwa la klabu za lottery kote ulimwenguni la kushirikiana na serikali na mashirika yanayofanya kazi ya kusaidia jamii ili kuziwezesha katika juhudi zao.

"Nikiwa kama mwakilishi wa kampeni klabu ya lottery kimataifa ya kumwezesha msichana nilivutiwa na kampeni ya namthamini kwa kuwa ina lengo ya kumsaidia mtoto wa kike kuendelea na masomo," alisema Aisha.

Vile vile, alisema kupitia programu yao ya kuwapa ufadhili wa masomo ya elimu ya juu mabinti wa kitanzania tangu mwaka 2010, wamegundua kuwa wasichana wengi hawamalizi masomo ya sekondari kutokana na kukosa taulo za kujisitiri wanapopata hedhi.

"Wasichana wengi hawana uwezo wa kuomba ufadhili huu kwa sababu hawamalizi elimu ya sekondari. Na hawamalizi elimu ya sekondari kwa sababu wanakumbana na changamoto ya kutafuta taulo za kike kila mwezi," alisema.

Alisema bado wanaendelea kukusanya michango kwenye matawi mengine ili wachangie pedi zaidi zitakazowawezesha wasichana 1,200 kuhudhuria masomo mwaka mzima.

Mwenyekiti wa Kampuni ya IPP, Abdiel Mengi, aliishukuru klabu hiyo kwa kushirikiana nayo kufanikisha kampeni ya namthamini iliyolenga kuhakikisha kuwa hedhi haiwi kikwazo cha mabinti kukosa masomo.

Alisema kampeni hiyo ni moja ya programu za kumnyanyua mwanamke zinazofanywa na kampuni ikiwa ni shauku ya muda mrefu ya kurudisha fadhila kwa jamii.

Meneja Uhusiano wa Wateja East Afrika Televisheni na Radio, ambaye ni Meneja wa mradi huo, Nancy Mwanyika, aliishukuru klabu hiyo kwa kuwapatia misaada hiyo na kuwa mchango huo utaweka shule jumla ya wasichana 800 mwaka mzima.

"Kwa niaba ya East Africa Television na Radio, tunapenda kuwashukuru klabu ya lottery msaada tulioupokea leo na mingine waliotuahidi kutoa," alisema Nancy.

Alisema katika kampeni hiyo wanashirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na mwaka huu wanatarajia kuwafikia wasichana walipo kwenye mikoa ya Mtwara, Njombe na Ruvuma.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **14.06.2022** hadi **27.06.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili:

**KCJ943F/ZE1097, KCM104W/ZF0174**
**KBQ622Z/ZE0978, KCK293W/ZE2585**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
**Urefu - Mita 21** **Upana - Mita 4.15** **Kimo - Mita 5.15**

3. Njia itakayotumika: **Holili** hadi **Moshi** kupitia **Soweto**, gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

216998001




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba (kulia), Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui (katikati) na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Stephanie Mouen (kushoto), wakionyesha wanahabari na wadau walioshuhudia utiwaji saini mikataba ya mkopo wenye masharti nafuu wa Sh. bilioni 195 uliotolewa na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufaransa yatoa mabilioni katika mradi wa majisafi

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI ya Ufaransa kupitia Shirika la Maendeleo la (AFD), imeipatia Tanzania mkopo wa Euro milioni 75 (Sh. bilioni 195), utekelezaji wa mradi wa usambazaji majisafi na usafi wa mazingira mkoani Shinyanga.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema hayo wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba wa mkopo huo kati ya Tanzania na Ufaransa, jijini Dar es Salaam.

Tutuba aliwashukuru AFD kwa kuwa miongoni mwa wafadhili wakubwa wa sekta ya maji na usafi wa mazingira nchini, akibainisha kuwa wanachangia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo endelevu ya maendeleo ya milenia ya Umoja wa Mataifa (UN) ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji safi kwa wote kufikia 2030.

"Kwa niaba ya serikali napenda kutoa shukrani zangu kwa serikali ya Ufaransa na AFD kwa ufadhili huu, lengo kuu la mradi huu ni kutoa huduma za uhakika na endelevu za upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira Manispaa ya Shinyanga na kuchangia kuboresha afya," alisema na kuongeza;

"Mradi huu pia utaboresha ustawi wa jamii na hali za maisha ya wanufaika, miundombinu iliyoko na ufanisi wa uendeshaji na utoaji wa huduma bora kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA)," alisema Tutuba.

Aliongeza kuwa hiyo ni moja ya ajenda kubwa inayoendana na hatua za serikali chini ya mpango wa tatu wa taifa wa miaka mitamo unaoanzia 2021/22 hadi 2025/26 unaotoa vipaumbele ikiwamo kuboresha upatikanaji na usambazaji wa maji na huduma za usafi wa mazingira, utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira mijini na vijijini.

Alibainisha kuwa ufadhili huo wa AFD utachangia pia kufikia moja ya vigezo vya mpango wa tatu wa miaka mitano na ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 ya kuongeza asilimia ya watu wa mijini wanaopata huduma ya majisafi.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema maji ni muhimu katika kila malengo ya maendeleo endelevu, serikali yake imejizatiti kufanya kazi na Tanzania kwa lengo la kuchochea maendeleo endelevu hasa katika sekta ya majisafi na usafi wa mazingira, kilimo na uzalishaji.

Mkurugenzi mkazi wa AFD nchini, Stephanie Mouen, alisema lengo kuu la ufadhili huo ni kuboresha hali ya maisha ya wakazi, mazingira, pamoja na maendeleo ya kiuchumi ya jiji kupitia upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji ya kunywa na huduma za usafi wa mazingira.

"Mradi huu unalenga kutoa huduma endelevu ya upatikanaji wa maji bora kwa asilimia 95 na ufikiaji wa huduma za usafi wa mazingira kwa angalau asilimia 45 ya wananchi ifikapo 2025 pamoja na kutoa msaada wa kiufundi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na kujenga uwezo wa SHUWASA," alisema Mouen.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, aliishukuru AFD kwa ufadhili, akibainisha kuwa utekelezwaji wa mradi huo utawezesha upatikanaji wa majisafi kwa zaidi ya asilimia 95 na wanaishukuru serikali kwa kuwajali wananchi kuwaboreshea huduma za kijamii.

"Nimshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira wezeshi ya nchi yetu kuaminiwa na nchi mbalimbali na rafiki ambazo zinatukopesha kwa masharti nafuu ili kutekeleza miradi hii ya kimkakati katika maeneo tofauti," alisema Sanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Mhandishi Yusuph Katopola, alisema utekelezaji wa mradi huo utasaidia kuzalisha ajira na kukuza uchumi wa mkoa mzima wa Shinyanga na kuufanya uwe na uchumi imara.

"Sekta ya maji ni muhimu katika maendeleo ya shughuli zote za kiuchumi, Shinyanga tuko tayari kufanya kazi bila kuchoka wakati wote wa utekelezaji wa mradi huu na kuhakikisha kwamba unakamilika ndani ya muda na kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyowekwa kwenye mradi," alisema Katopola.

## Atuhumiwa kumuua mzazi kwa kumcharanga na kumtoa utumbo

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Kulwa Meneja (34), mkazi wa Kijiji cha Ilelema Halmashauri ya Msalala wilayani hapo, kwa tuhuma za mauaji ya mama yake mzazi Magreth Makenzi (54), kwa kumkata panga tumboni hadi utumbo kumwagika na kusababisha kifo chake.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Shilela, Mwanaidi Mzee, alisema mwanamke huyo aliuawa akiwa amelala baada ya mtoto wake kumvamia chumbani na kutekeleza unyama huo.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa akiwa na mwenzake aliyejulikana kwa jina moja la Busheni, walivamia nyumba hiyo, kubomoa mlango na kuingia chumba alichokuwa amelala na kutekeleza mauaji hayo.

"Ni kweli tukio hili limetokea Juni 12, saa 6:20 usiku na mama huyo alikatwa panga tumboni na mwanawe na utumbo kutoka nje, mama alipoteza maisha papo hapo," alisema Mwanaidi.

Alisema tukio hilo lilitokea muda mfupi baada ya kikao cha familia cha msiba wa mjukuu wa marehemu kumalizika saa sita usiku.

Mwanaidi alisimulia kuwa majirani wa marehemu walisikia kishindo cha kubomolewa kwa mlango na walipotoka waliona watu wawili, mmoja akiwa mtoto wa marehemu na mwingine rafiki yake akitokea ndani huku mtoto huyo akifoka ovyo.

"Majirani waliingia chumbani na kukuta mama tayari amefariki na utumbo umemwagika chini huku baba yao mzazi akiwa amepigwa butwaa bila kuzungumza chochote ndipo walipopiga kelele na watu wakafika," alisema.

Alisema mtuhumiwa baada ya mauaji hayo alimpigia simu mwenyekiti wa kitongoji hicho akidai kuwa yupo porini amejificha kwa kile alichodai ndugu zake wamepanga kumuua kwa madai amemuua mama yake.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nkonze, Nchepe Eliasi, akizungumzia tukio hilo alisema siku hiyo alipigiwa simu majira ya saa sita usiku na jirani wa familia hiyo aliyemwambia kuwa familia ya jirani wanalia wakiashiria kuna tukio kubwa, anaomba msaada wa haraka ili kujua kilichojiri.

Muda mfupi, Mwenyekiti huyo alisema, kijana anayetuhumiwa kufanya mauaji hayo alipiga simu kuwa akidai yupo porini ameona gari lake (mwenyekiti) likipita na alikuwa akiomba msaada wake.

Alisema alimtaka mtuhumiwa huyo aendelee kukaa porini mpaka vurugu ziishe ili amfuate kwa ajili ya kupata ufumbuzi. Baada ya viongozi wengine kufika eneo la tukio alimfuata na kumrejesha nyumbani kwa ulinzi mkali ili asiuawe.

"Nilipofika porini ambako kajificha, kijana huyo akadai kuwa anaonewa anahusishwa na mauaji ya mama yake na kunitaka nimwangalie kama ana damu. Nilimulika tochi na kugundua shati lina damu, lakini nikamdanganya kuwa halina damu na nikamwambia nitamchukua na kumficha ndani."

"Mpaka tunaingia ndani watu hawakujua nimeingiza mtuhumiwa, nikamwekea ulinzi ili asijinyonge na wala wasiingie ndugu wakabaini ni yeye yakatokea mauaji mengine. Mpaka walipokuja polisi ndipo nikamtoa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kubanwa na askari hao kwa ushirikiano wake na kumwahidi akisema ukweli watamkabidhi Shilingi milioni moja. Alisema mtuhumiwa alikiri kazi hiyo wameifanya wawili lakini mwenzake amekimbilia Chato, mkoani Geita nyumbani kwao.

"Mtuhumiwa alikiri kwamba amefanya kitendo hicho kwa hasira kutokana na mama yake kumsumbua kwa uchawi kwamba aliroga ng'ombe wake wawili wakafa na mpaka sasa anahangaika kwa waganga wa kienyeji kutokana na mtoto wake kusumbuliwa na maradhi ya muda mrefu," alidai mwenyekiti.

Alisema mtuhumiwa aliendelea kufunguka kuwa kila alipoenda kwa waganga kupigiwa ramli, alibaini mama yake ndiye anayehusika.

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa watoto wa familia hiyo, Shija Meneja, alidai kushuhudia kaka yake akitoka ndani katika nyumba ya mama yake akiwa na mwenzake.

"Kama kawaida ya ukoo baada ya msiba tulikaa kikao mpaka saa sita usiku na kwenda kulala tukijiandaa kwamba kesho yake tuanze kurudi makwetu, mara saa sita tulipoingia kulala tukasikia kishindo kama kuna mtu kafungua mlango kwa nguvu tukadhani ni baba katoka nje tulipojiridhisha mimi na wenzangu kufungua mlango kumbe ni kaka na mwenzake wametokea ndani kwa wazazi wetu, alisema. "Kwa hali waliyokuwa nayo, tulimuona kaka akidai hii ni dharau kabisa, tukahisi tumevamiwa na kwa kuwa hatukuwa na silaha tulirudi ndani wapite kwanza, baada ya kuridhika wametokomea tukaingia ndani kwa wazee ili tuhoji kaka amekuwaje? Ndipo tukakuta mama kafariki na utumbo wote umemwagwa chini huku baba naye hajitambui kutokana na kupata mshtuko."

Meneja alidai kuwa walipomhoji baba yake kulikoni alidai kwamba wauaji walimwamuru ajifunike shuka usoni na asitazame kinachoendelea.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwa wanamshikilia kijana huyo huku upelelezi ukiendelea kumnasa mtuhumiwa wa pili wa mauaji hayo.

# Bilioni 972/- kuboresha mfumo elimu ya juu

Na Jenifer Gilla

SERIKALI na taasisi za elimu ya juu nchini zimesaini makubaliano utekelezaji wa mradi wa elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET), uliotokana na mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 425 (Sh. bilioni 972) kutoka Benki ya Dunia (WB).

Akizungumza katika utiaji saini huo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema fedha hizo mkopo huo unaleta mageuzi ya kiuchumi kupitia elimu ya juu.

Waziri Mkenda alisema mradi huo wa miaka mitano utafufua na kupanua uwezo wa vyuo vikuu ili kuchangia maeneo muhimu ya ubunifu, maendeleo ya kiuchumi na umuhimu wa soko la ajira, kwa kuwekeza katika mahitaji, miundombinu kwa ajili ya ufundishaji na utafiti wa kisasa na wenye ufanisi.

Kwa mujibu wa Prof. Mkenda mradi huo unalenga kufikia matokeo ya kimkakati ya kuongeza uandikishaji katika fani za kipaumbele, kuboresha umuhimu na ubora wa programu katika vyuo vikuu ili kukidhi hali na viwango vya soko la ajira la sasa na la baadaye.

Matokeo mengine yaliyokusudiwa ni pamoja na kuimarisha uratibu, usimamizi na kanuni za ngazi ya mfumo ili kuhakikisha wingi, ubora na umuhimu wa elimu ya juu nchini Tanzania, na kuongeza kiwango cha kuajiriwa kwa wahitimu kwa kuboresha umuhimu wa mitaala na kuunda mipya na inayoendeshwa na mahitaji.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema jumla ya taasisi 23 zitanufaika na mradi huo ikiwamo vyuo vikuu 14, taasisi tatu zilizomo chini ya Wizara ya Elimu na vyuo vinane vilivyoko chini ya Wizara ya Fedha.

Pia alisema mradi huo umelenga kupunguza matatizo ya elimu ya juu utafiti kuonyesha kuwa bado taasisi hizo zina matatizo hayo ikiwamo upatikanaji wa fedha za kugharamia mfumo wa elimu ya juu na upatikanaji wa elimu bora.

Aliitaja miongoni mwa mikoa inayotarajiwa kunufaika na mradi huo kuwa ni Lindi, Ruvuma, Rukwa, Songwe, Simiyu, Kigoma Tabora, Shinyanga na Singida. Mingine ni Dodoma, Kagera, Mwanza, Tanga, Mara, Manyara na Katavi.

Benki ya Dunia ilitekeleza mradi huo mwaka 2021 na vyuo vikuu vinatarajiwa kufungua kampasi mpya katika mikoa 17 na kuanza mafunzo ya programu maalum.

Mwakilishi wa Mkurugenzi mkazi wa Benki ya Dunia, Nkahiga Kaboko, msimamizi wa mradi huo, alisema mradi huo wa miaka mitano utabadilisha sekta ya elimu nchini kwa kuboresha mfumo wa elimu ili uendane na soko la ajira.

Alisema benki hiyo imejipanga kuhakikisha mradi wa HEET unafanikiwa na nyenzo zimetayarishwa ili kuongoza utekelezaji wake, kwa kuzingatia Sera za Ulinzi za Benki ya Dunia.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# VACANCIES ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is implementing its five years Corporate Strategic Plan (2022/2023-2026/2027) which includes the network expansion in local, regional and international destinations as well as improvement of its internal operations and human capital management. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the positions mentioned below as follows: -

**1. Position: Senior Internal Auditor I (1 POST)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Holders of Bachelor degree in Accounting/ Finance Management
- Holder of CPA (T) and registered with NBAA
- Postgraduate qualifications and sound computer application skills will be an added advantage.
- Direct appointment requires holder of Relevant Certificate with at least five years' work experience in internal or external auditing.
- Working in aviation industry is an added advantage
- CFE/CIA/CISA Certifications is an added advantage

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Prepare and arrange for contact with client and execute all required meetings for the allocated audit engagement.
- Review audit tentative programs, internal control and risks and engagement plan
- Administer and coordinate activities of the allocated audit engagement
- Evaluate the adequacy and effectiveness of the controls in the audited areas
- Develop comprehensive practical programs and schedules for Audit Coverage Areas.
- Review all documented audit findings and ensure their effective communication to the client and obtain responses
- Prepare draft and final audit engagement reports
- Schedule project and staff assignment to comply with management needs with scope of the department over all schedules
- Conducts special investigations as assigned by Chief Internal Auditor/ other relevant authorities
- Coordinate Audit schedules to avoid conflict with the external Auditors work
- Assists in the preparation of annual budget and Annual internal audit plan for the unit
- Performs any other duties as may be assigned by superiors.

**2. Position : Internal Auditor II – Financial (1 POSTS)**

**2.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:**

- Holder of Bachelor degree in Accounting/ Finance Management
- Holder of CPA (T) and registered with NBAA
- Sound computer application skills will be an added advantage.
- Working in aviation industry is an added advantage
- Direct appointment requires holder of Relevant Certificate with at least three years' work experience in Internal and External Auditing
- CFE/CIA/CISA Certifications is an added advantage

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**

- Identify and review all required information and document all controls and risks for internal audit planning
- Develops and execute audit programs as assigned by assignment team leaders
- Conducts audit to appraise the adequacy and use of financial, accounting and operating controls on each assigned engagement
- Conducts special investigations as assigned by Chief Internal Auditor/ other relevant authorities
- Prepares audit reports
- Document all audit working papers as per laid down guidelines on every audit engagement in the permanent and current files
- Participate on preparation of Annual Internal Audit plan
- Follow up on Audit recommendations
- Assists in the preparation of annual budget for the unit
- Performs any other duties as may be assigned by supervisor.

**3. REMUNERATION:**

Attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Scale and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**5. CLOSING DATES:**

Applicants should consider the following closing dates for each post as follows:

Within Fourteen (14) days from the first date of this announcement

The application letters should be directed to the following address: -

**Managing Director & CEO,**
**Air Tanzania Company Limited,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Advert date: 21ST June, 2022**

216910101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Imetosha unyama huu ukomeshwe

**WATANZANIA** wana mambo mengi yanayowasifia na kuwatofautisha na jamii nyingine duniani kama ukarimu, upole na upendo, lakini wana udhaifu unaoaibisha na kufedhehesha,

Mojawapo ni wizi wa mali za maiti wa ajali za barabarani na hata kuwaua majeruhi ili kuwapora mali zikiwamo fedha, vitu vya thamani na mizigo yao.

Uovu huo umekuwa na athari kama majeruhi ambao wangenusurika hospitalini kupoteza maisha baada ya kumaliziwa (kuuliwa) na waporaji. Lakini, majeruhi kukosa msaada kwa vile badala ya kuokoa maisha ya watu kwanza, wanaofika eneo la tukio wanaanza kupora na kukimbilia vitu ili kuiba mali nyingi lakini si kuokoa binadamu wenzao wanaohitaji msaada.

Athari nyingine ni miili ya ajali kutokutambuliwa hospitalini na kuzikwa na serikali, yote hayo ni kwa sababu vitambulisho vyao vimeporwa na pengine jamaa zao hawakuwa na taarifa za shughuli za ndugu hao iwapo walisafiri.

Ni fedheha kwa taifa pale gari linapopata ajali watu wanaanza kuwaweka majeruhi na marehemu pembeni na kuwapekuwa. Wanawaibia simu, pochi, waleti, saa, mavazi ya thamani, mikanda, mizigo yao na pale inapoonekana majeruhi analeta upinzani anaumizwa zaidi hata kuuawa.

Uporaji hauishii hapo kuna madai kuwa gari nalo huchokonolewa zikaibiwa betri, taa, redio na vifaa muhimu na kama ni usiku hata injini na matairi vinaweza kuibwa.

Wizi wa kupora wafu na majeruhi tena kuwaua ni tabia inayokomaa, kama taifa kinachosikitisha ni kukosekana sauti za mara kwa mara za kutaka kuwe na sheria ya kuharamisha kuibia marehemu wa ajali zozote na majeruhi.

Tunaona kuwa ni wakati wa wadau na serikali kuangalia namna bora ya kudhibiti uovu huu kwa kutunga sheria.

Lakini, tungependa kuona watuhumiwa wa makosa hayo wakifikishwa mahakamani na kuadhibiwa kikamilifu ili kudhibiti mienendo hiyo inayokatisha kinyama maisha ya binadamu hasa wasafiri.

Inashangaza kusikia wapo Watanzania wenzetu wanaokaa kwenye vyumba vya kuhifadhi miili hospitalini kwa muda mrefu bila kutambuliwa na kuzikwa na jamaa zao, badala yake wanazikwa na mamlaka za manispaa na halmashauri za miji na majiji.

Tunajiuliza hivi kuna watu ambao hawana ndugu? Japo inatokea miili haikutambulika kisa haikuwa na vitambulisho, lakini hili ni jambo lisilokubalika.

Tunaoimba serikali ijitahidi kuweka kamera za kurekodi matukio za CCTV kwenye barabara kuu zote kuanzia Dar es Salaam hadi mikoani zinapoishia. Ni vyema pia halmashauri za majiji, miji na manispaa mikoani na wilayani nazo zikaweka CCTV kamera kurekodi hali ya usalama barabarani na kudhibiti uhalifu ukiwamo kuwaibia majeruhi, kuwaua na kuwapora wafu badala ya kusaidia na kuokoa maisha yao.

Wadau wasikae kimya wakiwamo asasi za kiraia za kutetea wasafiri, usalama wa abiria na Jeshi la Polisi wakati wa kampeni ya Wiki ya Usalama Barabarani, isiishe kukagua magari wawe wabunifu na kuzungumzia haki ya abiria aliyepata ajali.

Wawakumbushe vijana na kuhamasisha kuhusu usalama ukiwamo haki ya maisha ya majeruhi wa ajali za barabarani na ulinzi wa mali zao.

Inavyoelekea mazoea ya kuibia majeruhi yamekuwa na sasa ni jambo linalokubalika kama wanavyofaniwa wezi mitaani.

Inaelekea kuwa ni jambo la kawaida mwizi kuteswa, kupigwa na kuchomwa moto.

Hivi mienendo hiyo ni sahihi? Kwanini tabia hizo ziendelee miaka na miaka za kuua watu kisa kelele za mwizi na kumfukuza wanayemuona mbele yao bila kuwa na uhakika.

Tunashauri mambo hayo yaanze kukemewa na kukomeshwa si jambo jema kuuana si vibaka, majeruhi wa ajali barabarani wala kuiba mali za wasafiri baada ya vyombo vya moto kupinduka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Dainess Mwakaje, SJMC

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulea watoto ipasavyo ni kukuza uchumi

**TAKWIMU** za hesabu za watu za mwaka 2012 zinaonyesha kuwa Tanzania ina idadi kubwa ya watoto, hali inayolielekeza taifa kuwekeza zaidi kwenye maendeleo ya kundi hilo.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 idadi ya raia ilikuwa milioni 45, lakini ikibainisha kuwa asilimia 44 ya Watanzania hao ni watoto ambao wana umri chini ya miaka 15.

Uwekezaji kwa watoto ni kuhakikisha kuwa wanakuwa na afya bora, wasio wadumavu, wasio na maradhi, wenye elimu na malezi bora, wanaolindwa dhidi ya vurugu, udhalilishaji na unyonyaji hasa kutumikishwa kwenye ajira haramu.

Ni wazi kuwa kila nchi iliyofikia kuwa na maendeleo ya kiuchumi ya kipato cha wastani imewekeza kwa watoto kwa kiwango kikubwa.

Hivi sasa kuwekeza kwa watoto kwenye elimu bora, huduma za jamii ziliimarishwa na kuwalinda watoto dhidi ya vurugu na udhalilishaji huzaa matunda kama uchumi imara kutokana na nguvu kazi, taifa lenye afya na kupungua uhalifu.

Serikali inafanya juhudi kama kuanzisha utaratibu wa kuwapatia bima ya afya watoto na kila mtoto anayezaliwa anapata kadi ya matibabu ili kusaidia kwa jitihada za kuwa taifa lenye afya bora huku ikigharamia elimu ili wasome na kuwa na kuepuka ujinga.

> **Ni wazi kuwa kila nchi iliyofikia kuwa na maendeleo ya kiuchumi ya kipato cha wastani imewekeza kwa watoto kwa kiwango kikubwa.**

Maendeleo makubwa yanahitajika kwa watoto huku jamii zikihamasishwa, kuongeza uwajibikaji na uwazi kuhusu ulinzi kisheria na kusimamia miongozo yote inayohusu ustawi wa watoto na kuhakikisha kuwa inatekelezwa kikamilifu ili kuwalinda.

Matumizi mazuri ya rasilimali zilizoko kwa kuboresha huduma muhimu na kuimarisha fursa kwa watoto kutaziwezesha familia nyingi kujitoa katika umaskini na kuwa na watoto wenye afya na ustawi bora.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Umoja wa Mataifa linashughulikia Watoto Duniani (UNICEF) vifo vya watoto vimepungua nchini kwa asilimia 25 na Tanzania inaendelea vizuri kuelekea kwenye lengo la maendeleo ya milenia kuhusiana na kutunza uhai wa watoto wachanga.

Hata hivyo, zaidi ya watoto 445 walio chini ya umri wa miaka mitano hufariki kila siku na zaidi ya watoto 140 kati yao ni wachanga ambao hawajatimiza mwezi mmoja.

Kadhalika, kila saa moja kuna mwanamke anayefariki kutokana na matatizo yanayohusiana na uzazi, hivyo serikali inapaswa kuwekeza zaidi kwenye huduma za afya kuokoa maisha ya maelfu ya wananchi.

Serikali inahitajika kuweka mfumo bora zaidi wa afya utakaokuwa na wafanyakazi zaidi, vituo vya afya vyenye vifaa vya kutosha, ufuatiliaji na usimamizi mzuri na uwajibikaji mkubwa, sera, sheria, miongozo na miundo yote inayohusiana na afya, itoe kipaumbele kwa wanawake na watoto.

Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yamekuwa yakishamili kila siku, yanasikika kupitia vyombo vya habari, mara mtoto kachomwa moto mikono, kafichwa kwenye boksi kwa miaka minne au kuuliwa na watumishi wa ndani.

Watanzania wanapaswa kutambua thamani ya mtoto kwa kuwalea na kuwatunza ipasavyo, kwani ukimlea mtoto vizuri leo, kesho atakuwa hazina ya familia na ya taifa.

Watoto wengi wenye ulemavu wananyimwa haki ya kupata elimu, baadhi hufungiwa ndani na kufanyiwa matendo ya 'kinyama'.

Ili kukabiliana na hali hiyo sheria zinazohusiana na watu wenye ulemavu zinapaswa kukamilishwa na kutekelezwa, wadau na wahisani mbalimbali washirikishwe ili kuwapo rasilimali za kutosha kuanzia fedha, wataalamu na watumishi kwa ajili ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuundwa chombo cha uratibu.

Upatikanaji wa huduma maalumu za watoto wenye maalumu unapaswa kuongezewa nguvu, ikiwa ni pamoja na mipango ya jamii ya kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida, vituo vya huduma vya matibabu mahususi na kuwa na wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ili watoto wote wenye ulemavu waweze kupatiwa huduma pamoja na vifaa wanavyovihitaji.

Mwisho, serikali inapaswa kukumbuka kuwa ule msemo usemao mtoto ni taifa la kesho umepitwa na wakati, bali mtoto ni taifa la sasa na mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

## Bashungwa: Uteuzi viongozi elimu uzingatie umahiri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ametoa maagizo matano ya kuhakikisha usimamizi wa elimu unaboreshwa nchini, mojawapo ni uteuzi wa viongozi wa elimu uzingatie umahiri na uzoefu.

Alitoa maagizo hayo jana jijini hapo wakati akifungua mkutano wa Umoja wa Maofisa Elimu Maalum Tanzania Bara (UMEMTA).

"Kuwapo kwa usimamizi usioridhisha kwenye usimamizi wa elimu kwa baadhi ya viongozi wa elimu. Baadhi ya viongozi wa elimu katika ngazi za shule, kata, halmashauri na mikoa kutozingatia majukumu yao ya kufuatilia kwa makini ufundishaji shuleni," alisema.

Alisema viongozi hao ni wasimamizi wa elimu ili kuleta tija katika usimamizi wa ufundishaji shuleni.

Aliagiza mkakati wa kuboresha elimu uundwe mara moja ili kuongoza namna bora ya utekelezaji wa mitaala nchini.

"Mkakati huu unalenga kuleta ufumbuzi wa nini kifanyike sasa katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Mkakati huo ukamilike ifikapo mwishoni mwa Julai, 2022," alisema.

Alisema inapaswa kubuniwa utaratibu bora wa kutumia rasilimali walimu katika shule ili kuwe na msawazo bora wa walimu usioathiri baadhi ya maeneo yenye upungufu mkubwa.

"Viongozi wote wanaosimamia elimu katika ngazi mbalimbali za shule, kata, halmashauri na mikoa kuhakikisha ufundishaji unaimarisha shuleni wenye kuleta matokeo chanya," alisema.

Aliwaagiza maofisa elimu kuendelea kusimamia na kuijengea jamii uelewa kuhusu upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

"Endeleeni kusimamia uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule zinazopelekewa fedha. Serikali na wadau wengine ili ziwe rafiki kwa wanafunzi wote wakiwamo wanafunzi wenye mahitaji maalum," alisema.

Katibu wa umoja huo, Joshua Samson, aliomba serikali kutoa posho kwa walimu wa elimu maalum nchini, huku akiwahimiza maofisa elimu kulipa madeni.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu, TAMISEMI, Hadija Mcheka, aliwataka kuendelea kuwaibua watoto wenye mahitaji maalum popote walipo kwa kuwa dhamira ya serikali ni kuhakikisha elimu inayotolewa nchini haibagui wala kuchagua.

# Mwinyi ahakikishia wadau mazingira rafiki

**Na Mwandishi Wetu**



RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali zote mbili zitaendelea kuandaa mazingira rafiki na kufanyakazi kwa karibu na wadau wote katika kuimarisha ustawi wa ujenzi wa wananchi.

Rais Mwinyi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozindua Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF).

Alisema hayo yanafanyika kwa kuwa jukumu la serikali ni kuandaa mazingira yatakayowezesha sekta binafsi na asasi za kiraia kushiriki katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Alisema programu za kuwezesha wanawake wajasiriamali, elimu na afya za EOTF ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Dk. Mwinyi alisema EOTF ni mdau muhimu wa serikali katika kuimarisha ustawi wa watoto, vijana na wazee wa jinsia zote.

Naye Mwenyekiti wa Mfuko huo, Mama Anna Mkapa, alisema kwa miaka 25 wamekuwa mstari wa mbele katika nyanja ya kuuondoa umaskini kwa wanawake kwa kuwawezesha wajasiriamali 6,000 kutoka Bara na Visiwani kupata mafunzo ya ujasiriamali.

Pia alisema wamesaidia kutangaza na kukuza bidhaa zao kupitia maonyesho mbalimbali na kujipatia zaidi ya Sh. trilioni 11, ikiwa ni pamoja na kuzalisha ajira zaidi ya 25,000.

Programu nyingine aliyoitaja ni kusaidia kwenye elimu kwa kuwa imetoa ufadhili kwa watoto 1755 kutoka kwenye familia duni kupata elimu ya chekechea, msingi, sekondari, Veta hadi vyuo vikuu ndani na nje ya nchi.



Ndege waliopachikwa jina la 'bwana afya' kutokana na kula mabaki ya samaki yanayotupwa na wafanyabiashara wa eneo la Kamanga, jijini Mwanza, wakisubiri mabaki hayo hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wanaume wamlalamikia DC kunyanyaswa kijinsia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAUME wa Kijiji cha Igominyi, Kata ya Yakobi Halmashauri ya Mji wa Njombe, wamelalamika unyanyasaji wa kijinsia wanaofanyiwa na wanawake na kusababisha baadhi yao kujiua.

Akizungumza katika ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Gwakisa, mmoja wa wananchi hao Elisha Nyagawa alidai, wanawake wengi kijijini hapo wana tabia za kuwanyanyasa wanaume zao kwa kufanya mahusiano na wanaume wengine kwa tamaa ya fedha.

Alisema tabia hiyo imeibua simanzi kwa jamii na wanaume hukaa kimya bila kuripoti matukio hayo ya kunyanyaswa.

"Katika kijiji chetu wanawake wamekuwa wakiwanyanyasa sana wenza wao wanaume, tatizo kubwa ni kuwa kama mwanaume huna hela mwanamke anatafuta mwenye hela. Hii inasababisha wanaume katika kijiji chetu kujiua kutokana na sababu hiyo, halafu hapa kijijini wanasema kuwa kama hauna hela muite mkeo shemeji," alidai Nyagawa.

Akizungumzia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya aliwataka wanaume kuvunja ukimya na kuripoti matukio hayo kwa kuwa serikali imeanzisha madawati ya kijinsia kwa ajili ya kuwahudumia wanawake na wanaume wanaokumbana na matatizo hayo ya ukatili.

"Jamii itusaidie tusiruhusu wenza wetu wakapoteza uhai wao kikatili hivyo, kwa maana kesi za kujinyonga kwa msongo wa mawazo, na sisi kinamama tusichukulie jambo hili kuwa ni jepesi linaharibu afya ya akili ya wenza wetu. Serikaili imeanzisha madawati yapo pale polisi twende ili kupata suluhu ya yale tunayokumbana nayo," alisema Kissa.

Kaimu Mkuu wa Polisi (OCD), Wilaya ya Njombe Magreth Mbawa, alisema kuwa wanaume wengi wanafanyiwa unyanyasaji wa kijinsia, lakini hawayaripoti matukio hayo Jeshi la Polisi kwenye madawati ya kijinsia kwa kuhofia kudharaulika katika jamii na kuonekana kuwa wao ni dhaifu.

"Madawati yapo kwa ajili ya jinsia zote, kinababa wanadhani kuwa madawati haya ni kwa ajili ya wanawake pekee, hapana. Wanaume wengi wananyanyasika kijinsia, lakini wengi ni wasiri wakidhani kuwa wakienda kuripoti polisi au kwa mwenyekiti wa kijiji au mtendaji ni aibu, hebu tufunguke tuseme," alisisitiza Magreth.

# NBS yawajengea uwezo wahariri uhamasishaji sensa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imewataka wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhamasisha wananchi kujitokeza kushiriki katika sensa ya watu na makazi inayofanyika mwaka huu.

Mtaalamu wa Habari na Mawasiliano kutoka Ofisi ya NBS, Said Ameir, alisema hayo wakati wa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu maandalizi ya sensa hiyo, inayotarajiwa Agosti 23, 2022.

Alisema wahariri ni moja ya kundi muhimu kuweka uelewa kwa wananchi kushiriki katika sensa na kwamba wanapaswa kutumia kalamu na vyombo vyao kutoa uelewa kwa wananchi umuhimu wake.

Akizungumzia mafunzo hayo alisema, wahariri wa vyombo vya habari wanajengewa uwezo ili waijue Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Sheria ya Takwimu, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 na umuhimu wake.

Pia, wanajengewa uwezo wa sensa hiyo maeneo ya kuhesabia watu, vyanzo vya uripoti, mbinu na mambo ya kuzingatia.

Eneo lingine ni changamoto za uripoti wa sensa kwa vyombo vya habari pamoja na njia za kusafisha na kuzibadili takwimu katika mfumo rafiki (Data Scraping & Cleaning), uchambuzi wa takwimu kwa ajili ya habari (Interviewing data au data analysis).

Alisema wahariri hao wanajifunza namna ya uwasilishaji wa takwimu za sensa kwa michoro (Census Data Visualisation), sensa katika mitandao ya kijamii na wajibu wa vyombo vya habari katika kufanikisha.

Akizungumza kwa niaba ya wahariri hao, Mjumbe wa Bodi ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Said Salim, alisema mafunzo hayo yameleta uelewa mpana katika mpango huo wa serikali.

Alisema wamebaini takwimu ndio kiungo kikubwa cha kuleta maendeleo kwa wananchi na kuahidi wanaporudi katika ofisi zao kwenda kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa.




Kaimu Mkuu wa Chuo cha Bahari (DMI), Tumaini Gurumo, akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa kimataifa kuhusu uchumi wa buluu unaofunguliwa leo na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (hayupo pichani). Kulia ni Makamu Mkuu wa chuo (Utawala), Dk. Lucas Pastory na Makamu Mkuu (Fedha), Jonson Kileo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# DMI yapigia chapuo mafunzo ubaharia

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Bahari (DMI), kimewataka Watanzania kuchangamkia fursa ya mafunzo ya fani ya ubaharia ambayo ina soko kubwa la ajira nchini na mataifa mbalimbali duniani.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Tumaini Gurumo, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini.

Akizungumzia mkutano wa mabaharia katika kongamano la kwanza la uchumi wa buluu litakalofunguliwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, litakalohudhuriwa na mabalozi wa nchi mbalimbali zenye bahari.

Alisema ubaharia ni fani kama zilivyo fani zingine zenye heshima ambayo husomewa kwa nadharia na vitendo na hatimaye mhusika akifaulu hupata cheti na kupanda madaraja kama ilivyo kwa fani zingine.

Alisema mafunzo yanayotolewa na DMI yana ithibati ya kimataifa na baharia anayefundishwa na chuo hicho ana uwezo wa kufanya kazi ndani ya nchi na kwingine kote duniani kwa kuwa vyeti vyake vitakuwa vinatambuliwa kimataifa.

"Uhitaji wa mabaharia duniani bado ni mkubwa sana wanahitajika wengi sana na nchi nyingi zina meli, lakini hazina mabaharia. Ukraine ilikuwa inatoa mabaharia wengi sana, lakini katika kipindi hiki cha vita hakuna mabaharia wengi wa huko wako nyumbani hivyo nafasi inazidi kuongezeka kwa mabaharia wa kitanzania," alisema.

"Fursa ni nyingi sana kwenye fani ya ubaharia nawaasa vijana, wazazi na walezi waitazame, fani hii zamani ilionekana kama vile ya kihuni, lakini leo hii imekuwa fani yenye uwezo wa kumwingizia mtu kipato kikubwa sana," alisema Tumaini. Alisema dhumuni la kongamano la siku mbili ni kupambanua fursa zinazopatikana kwenye uchumi wa buluu zilizoko baharini ili ziweze kutiwa vyema na Watanzania kwa maendeleo ya nchi.

Alisema mpango wa maendeleo wa miaka mitano ulioanza mwaka 2021-2025, umeweka bayana kwamba uchumi wa buluu ni kipaumbele katika shughuli za kuendeleza uchumi wa Tanzania.

Alisema kwenye kongamano hilo pia atahudhuria Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi wa Zanzibar ambaye atakuwa mmoja wa wazungumzaji wakuu kuelelezea fursa zilizoko.

"Tutasikia waziri wetu wa uchumi wa buluu anatuambia nini kuhusu fursa zilizoko kwenye uchumi wetu wa buluu hili ni kongamano la kwanza kabisa la uchumi wa buluu hivyo siyo la kukosa na siku ya kufunga tumepata fursa ya kuwa na Waziri wa Elimu, Profesa Adolth Mkenda," alisema Tumaini.

## Kwelea kwelea waharibu hekta zaidi 900 za mazao

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

NDEGE waharibifu wa mazao aina ya Kwelea kwelea wameharibu hekta 920 za eneo lililolimwa mazao sawa na asilimia 32 ya maeneo yote yaliyolimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singinda.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Natalia Mosha, alisema hayo wakati akizungumzia umwagiaji dawa ya kuua ndege hao waharibifu wa mazao, mchakato unaoendelea sehemu mbalimbali nchini.

Akizungumzia uharibifu uliosababishwa na ndege hao, Natalia alizitaja kata zilizoathiriwa zaidi kuwa ni Merya, Itaja, Ngimu na Mihunga za mkoani humo.

Alisema, umwagaji wa dawa hiyo ulianzia Kijiji cha Merya, Kata ya Merya na kwa sasa wanaendelea sehemu mbalimbali za mkoani Singida hadi ndege wote watakapoangamizwa.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo kutoka Kitengo cha Afya ya Mimea na Mazao- Wizara ya Kilimo, Laurent Zumba, alisema dawa imemwagwa katika maeneo wanayolala wadudu na kwa kuzingatia muda sahihi wa asubuhi au jioni ndiyo dawa inanyunyuziwa.

"Kweleakwelea ni ndege wanaopenda kushambulia mazao ya nafaka zikiwamo mpunga, ngano, mtama na uwele, ndege hawa hupendelea kulala maeneo tofauti na wanayotafutia chakula hivyo inahitaji uchunguzi ili kubaini maeneo wanayolala na ndipo ndege ya kumwaga dawa inaenda kumwaga kwa muda sahihi ambao ni asubuhi au jioni wakati ndege hao bado wapo," alisema Zumba.

Akiwazungumzia ndege hao, Zumba alisema, kweleakwelea mmoja ana uwezo wa kushambulia kati ya gramu tano hadi kumi kwa siku.

Alisema, wakiingia shambani kwa makundi hushambulia kwa haraka na kuhatarisha uwezo wa mkulima kupata mazao ya uhakika na kuiweka nchi kwenye hatari ya kuwa na uhaba wa chakula na ndiyo maana wizara inawakabili.

Noa wananchi wa Wilaya ya Singida vijijini wamepongeza uamuzi huo wa serikali wa kukabiliana na ndege hao kwa kuwa wamekuwa wakiwasababishia hasara kubwa.

Mkulima kutoka Kijiji cha Pohama, Kata ya Ngimu, Grabriel Said, alisema uamuzi huo wa serikali umerejesha imani kwa wakulima kuwa mazao yao hayataharibiwa tena.

"Namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwani serikali imesikia kilio chetu imeleta hii ndege ya kunyunyiza kiwatilifu kuangamiza kweleakwelea," alisema Said.

Naye mkulima, Hussein Juma, wa Kijiji cha Mtambaa alisema; "tulimsikia Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akisema kuwa ndege itakuja kuangamiza wadudu waharibifu na hakika hilo limeanza kutokea na nina imani kuwa mambo yanaenda kuwa sawa."

# Mkenda ataka ukuaji sayansi na teknolojia

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda, amesema kunahitajika msukumo mkubwa kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa mwaka wa Akademi ya Sayansi (TAAS), jijini Dar es Salaam.

"Sisi kwetu suala la sayansi na teknolojia bado linahitaji msukumo mkubwa sana, hasa natural science (sayansi asilia), engineering technology (teknolojia ya uhandisi), na wote tunajua nchi zetu zipo nyuma katika sayansi na matumizi yake, teknolojia na matumizi yake," alisema.

Alisema nchi inahitaji mwamvuli wa kuhamasisha masuala ya hayo na kuwaomba wana akademi hao kwa kuanzia waweke nguvu zaidi kwenye sayansi asilia, teknolojia na dawa.

Utekelezaji alisema katika bajeti ya mwaka 2022/2023 serikali imetenga Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwawezesha wanaofanya utafiti na kuchapisha majarida makubwa hasa utafiti wa asili na dawa.

"Na tumesema haijalishi mpo wangapi, wewe upo hapa Tanzania ni mhadhiri umeshiriki, mmeandika watu 10 wengine wapo Ulaya wapo wapi tumekuona upo kwenye landscape umechapisha, kitita cha Sh. milioni 50 kinakuhusu katumie unavyotaka, ili tujenge mazingira kwamba utafiti unalipa," alisema Waziri Adolf.

Pia aliwaona wasomi hao kuona umuhimu wa kuwajumuisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi waliobobea katika fani hiyo ili wasaidie vijana wa hapa nchini kupata ufadhili wa masomo katika vyuo vya nchi walizoko.

"Embu tuangalie uwezekano wa kuwa na mkutano na Watanzania waishio nje ya nchi katika akademi, kujadili namna ya kufungua fursa za Watanzania kwenda kusoma nje ya nchi, kwa sababu kwa kujifungia tu humu nchini hatuwezi kufika, tunahitaji kujifunza kutoka kwa wengine," alisema.

Aliwasihi Watanzania kuchangamkia fursa za ufadhili wa masomo nje ya nchi kwa sababu zipo nyingi, lakini mwitikio ni mdogo na kusisitiza kuwa mhadhiri wa chuo kikuu akipewa ufadhili na kukataa kwenda atafute kazi mahali pengine.

Akimkaribisha Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu wa Akademi ya Sayansi, Prof. Eliud Lyamula, alisema ilianzishwa kwa lengo la kuwa kitovu katika ubora wa uendelezaji na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya kijamii uchumi.

"Katika kutekeleza azma hii akademi imeandaa mpango mkakati ambao una malengo ya kati, ikiwamo kuongeza idadi ya wanachama, uwezo endelevu wa kifedha, kiutawala, rasilimali watu na miundombinu na ushirikiano kwenye masuala ya sayansi," alisema.

Alisema pia wananuia kuongeza ubora wa sayansi, teknolojia na ubunifu kitaifa, kuifanya sekta hiyo kuwa sehemu ya sekta ya kijamii uchumi na umma kwa ujumla na kuimarisha upatikanaji wa ushauri wa kisayansi.

"Mafanikio ya utekelezaji wa mpango wetu yanatarajia kuimarisha ushirikiano wetu na serikali pamoja na wadau mbalimbali," alisema.



Wananchi wa Kata ya Mabwepande Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam wakipika baada ya nyumba zao kubomolewa mwisho mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yashauriwa kuangalia kodi wenye miaka 18

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeshauriwa kuangalia kodi inayogusa watu wa kuanzia miaka 18, kwa madai ikianza kutozwa itasababisha usumbufu.

Ushauri huo umetolewa na Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), katika mkutano wake na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, hata hivyo, alipongeza bajeti ya nchi ya mwaka 2022/2023, kuwa ni ya kipekee kwa kupunguza matumizi ya serikali, lakini tatizo litakuwa kwenye kodi.

Alisema, kupitia bajeti hiyo, serikali inakusudia kuongeza mapato yake yatakayotumika kwenye maendeleo na huduma za jamii, lakini shaka la taasisi hiyo ni kuhusu kodi iliyopendekezwa na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba.

"Ushauri wetu kwa serikali ni kwamba ingeangalia sehemu nyingine ya kupata kodi hiyo, kwa kuwa vijana wa miaka 18, wengi wako sekondari au vyuoni, bado wanawategemea wazazi wao au walezi," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya alifafanua kodi hiyo inaweza kuweka kwenye mafuta ya dizeli na petroli kwa wamachinga na hata kwa malori ili kuepusha usumbufu kama ilivyotokea wakati wa kodi ya kichwa.

"Kuna watu wanafanya biashara kubwa, lakini wamejificha kwenye mwamvuli wa umachinga, hivyo kodi hiyo iliyoondolewa wakati wa serikali ya awamu ya tatu ingeelekezwa kwao," alisema.

Aliwataka wabunge kujadili kwa kina suala la kodi hiyo ili nchi isirudi kule ilikotoka ambako kodi hiyo ilisababisha watu kukimbia miji yao kukwepa kuilipa huku serikali ikitumia gharama kubwa kuikusanya.

"Hata kama njia inayopendekezwa kutumika ni ya simu, bado usumbufu unaweza kuwapo kama zamani, ukiwamo wa kuwasaka wale wanaomiliki simu, lakini hawaweki fedha kwa kuhofia makato ya kodi," alisema.

Pia, alishauri wazee waingizwe kwenye mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na kila halmashauri nchini badala ya wanawake, vijana na wenye ulemavu pekee.

"CEGODETA tunashauri wazee wapewe asilimia nne halafu hizo sita zilizobaki zigawanywe kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu," alisema.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya CEGODETA, Zakiah Juma, alisema ipo haja ya kupata ufafanuzi wa kina kuhusu kodi hiyo, kwa madai watu wengi wanaamini kuwa ni kodi ya kichwa iliyoondolewa baada kuonekana kero kwa Watanzania.

"Serikali inasema, kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea atapewa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) na atakadiriwa kodi zake na kutumiwa kwa njia ya mtandao na kulipa kulingana na kipato chake. Lakini ukiangalia, vijana wengi wenye umri huo hawana kazi, bado wanaishi kwa wazazi, hivyo kodi hiyo inaweza kuleta usumbufu," alisema Zakiah.

Alisema, taasisi yao inaamini kuwa serikali ina nia njema, ila wanaona kuwa inaweza kukosa kodi hiyo kwa vijana wa kunzia miaka 18 hadi 25, kwa madai kwamba bado ni tegemezi.

# Tatizo mimba za utotoni Shinyanga lashamiri

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI 166 mkoani Shinyanga wamedaiwa kupewa ujauzito, huku 61 wakiozeshwa ndoa za utotoni.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka hospitali ya rufani mkoani Shinyanga, Prisla Mushi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki iliyopita katika Kata ya Lyabukande, wilayani Shinyanga kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Akizungumza kwa niaba ya Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani hapo, Lidya Kwesigabo, alisema bado kuna tatizo la matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kuitaka jamii kubadilika na kuacha vitendo hivyo.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia Julai, mwaka 2021 hadi Mei mwaka 2022 jumla ya watoto 4,656 wamefanyiwa ukatili mkoani hapa na kati ya hao wa kike ni 3,313 na kiume 1,341, mimba za utotoni zilikuwa 166 huku ndoa za utotoni zikiwa ni 61," alisema Mushi.

Kwa upande wake, Katibu Talawa wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, aliwasihi wazazi mkoani humo kuachana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kwa kuzingatia haki za watoto na kuwatimizia mahitaji yao ikiwamo haki ya kupata elimu.

"Natoa rai kwa wazazi, viongozi wa dini, serikali na kila mwanajamii, kutoa kipaumbele cha kwanza katika ulinzi wa mtoto, hawa ni taifa la kesho tukishindwa kuweka msingi mzuri wa malezi kwa watoto wetu tutahatarisha ulinzi wa nchi yetu, tunapaswa kuhakikisha watoto wetu wanalindwa, wanapata mavazi, chakula, maradhi bora na elimu," alisema Chambi.

Baadhi ya wadau wa masuala ya kupinga ukatili dhidi ya watoto ambao walihudhuria maadhimisho hayo, walisema bado wananchi wa mkoa huo wanahitaji kupewa elimu ili kuzifahamu haki za watoto pamoja na sheria za ulinzi wa mtoto ili kupunguza matukio ya ukatili..

**Akizungumza kwa niaba ya Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani hapo, Lidya Kwesigabo, alisema bado kuna tatizo la matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kuitaka jamii kubadilika na kuacha vitendo hivyo.**

HABARI BUNGENI

# ‘Hakuna uhusiano uchimbaji madini, upungufu samaki’

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kirusa, amesema hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya uchimbaji madini na upungufu wa samaki katika miti na maziwa.

Alitoa ufafanuzi huo bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Jumbe.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji uchimbaji wa madini kando ya mito na maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki.

Akijibu swali hilo, Dk.Kirusa alisema uchimbaji wa madini umegawanyika katika aina kuu mbili, uchimbaji juu ya ardhi na ule wa chini ya ardhi.

“Sheria ya Madini Sura 123 ambayo hairuhusu uchimbaji wa madini katika vyanzo vya mito na maziwa na endapo shughuli za uchimbaji zitafanyika kando ya mto au maziwa zitafanyika umbali wa mita 60 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 20 ya mwaka 2004,”alisema.

Aidha, alisema kabla ya shughuli za uchimbaji wa madini kufanyika katika eneo husika tathmini ya mazingira hufanyika na kutathmini athari za kimazingira ikiwamo viumbe hai pamoja vyanzo vya maji.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema utafiti uliofanyika Aprili mwaka 2018, Marekani ilionyesha kuwa sehemu zenye machimbo ya makaa ya mawe karibu na mito kuna upungufu wa viumbe wa majini kwa asilimia 53 ikiwamo samaki.

“Je, sisi serikali yetu imefanya utafiti huo na kuja na majibu haya? Sasa hivi tunaanza kuchimba makaa ya mawe pale Kiwira, Mto Kiwira na Songwe imeathiriwa kwa namna hiyo, je, ni hatua gani zinazochukuliwa na serikali ili kusiendelee kupatikana kwa athari hizo,”alihoji.

Dk. Kiruswa akijibu maswali hayo, alisema Tanzania haina uchimbaji wa madini kwenye maeneo ya mito au maziwa ambayo yanasababisha athari hiyo.

Hivyo, alimhakikishia mbunge huyo kuwa katika eneo la machimbo ya makaa ya mawe Kiwira, tahadhari zote za mazingira zimechukuliwa na hakuna athari.




Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA



Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, akichangia hotuba ya fedha ya bajeti kuu ya serikali mwaka 2022/2023 kwenye mkutano wa saba wa kikao cha 47 cha Bunge la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ataka elimu wananchi kudai risiti

MBUNGE wa Kyerwa (CCM), Innocent Bilakwate, ameitaka serikali iweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kudai stakabadhi za EFD kwa kuwa bado kuna mwamko mdogo.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alihoji kutokana na hali hiyo serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kudai stakabadhi.

“Wafanyabiashara wengi hawana mashine za EFD na zilizoko nyingi ni mbovu, serikali ina mpango gani wa kununua mashine na kusambazwa kwa wafanyabiashara wote ili kuongeza mapato,” alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alikiri kuwapo na mwamko mdogo wa wananchi kudai stakabadhi na wafanyabiashara kutoa stakabadhi hizo.

Alisema mikakati ya serikali ni kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha, huku akitoa wito kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuendelea kufanya hivyo.

“Niwaombe wabunge kutoa elimu kwa wananchi kudai risiti baada ya kununua bidhaa. Tutaangalia suala la kutoa mashine hapo baadaye,”alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka alihoji mpango wa serikali wa kuboresha stakabadhi za mashine za kielektroniki (EFD) ili zisifutike baada ya muda mfupi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande, alisema kufutika kwa stakabadhi za mashine za EFD baada ya muda mfupi kumesababishwa na matumizi ya karatasi zenye ubora hafifu.

Hata hivyo, alisema baada ya kubaini tatizo hilo, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kushirikiana TRA imeshatengeneza viwango vya ubora wa karatasi hizo vinavyotakiwa na sasa wanaendelea na usimamizi kuhakikisha karatasi zote zinakidhi ubora unaotakiwa.

Alisema: “Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, TRA imeboresha mfumo wa usimamizi wa mashine za EFD kwa kuuwezeshe kupokea taarifa zote za kila risiti inayotolewa na kuitunza katika seva zake na hivyo kuwezesha nakala ya risiti hizo kuweza kupatikana wakati wowote inapohitajika”.

# Wizara ya Kilimo yaagiza upitiaji miradi umwagiliaji

WIZARA ya Kilimo, imeagiza Tume ya Maendeleo ya Umwagiliaji kupitia miradi yote ya umwagiliaji nchini ili kufanya tathmini.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Msalala (CCM), Iddi Kassim Iddi.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema mradi wa Chela ni wa muda mrefu, kuhoji serikali lini itaweka fedha za ukarabati wa mradi huo wa umwagiliaji.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema kutokana na uwapo wa umuhimu wa kukarabati miradi ya umwagiliaji Wizara ya Kilimo imeagiza tume hiyo kufanya tathmini na kujua hali ya miradi hiyo na kuchanganua ipi inahitaji ukarabati wa mkubwa na mdogo au ya kuanza kujengwa upya.

Mavunde alisema: “Lengo la serikali ni kuhakikisha miradi hii inafanya kazi na inakuwa na tija kwa wananchi,”alisema.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa alihoji lini serikali itakamilisha ukarabati wa mradi wa umwagiliaji katika Bonde la Liyuni ambao ulianzishwa muda mrefu haujakamilika.

Mavunde akijibu swali hilo, alisema bonde hilo lipo kwenye mkakati wa Wizara ya Kilimo wa kuhakikisha wakulima wanawezeshwa kulima kilimo cha umwagiliaji.

Awali katika swali la msingi, Mbunge wa Same Magharibi (CCM), Dk. David Mathayo alihoji lini serikali itasaidia kukarabati na kuboresha mifereji ya Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge na Kirua katika Bonde la Mto Pangani ambalo ni muhimu kwa uzalishaji wa chakula.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mavunde alisema serikali inatambua umuhimu wa Bonde la Mto Pangani katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

“Bonde hili pamoja na skimu nyingine, pia linajumuisha skimu za Kirya, Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge, Kirua na Ruvuna kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro,”alisema.

Aidha, alisema kwa sasa serikali inaendelea na ujenzi wa skimu ya Kirya ambayo inatarajiwa kukamilika mwaka 2022/23.

Alisema katika mwaka wa fedha 2023/24 serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge na Kirua ili kujua gharama halisi za ukarabati na ujenzi wa skimu hizo.

Australia yaikunjulia Tanzania mikono kuwa mshirika TEHAMA



Ukurasa 13



Ukurasa 13

## M-Mama inavyomweka 'rahani' mjamzito, mtoto

Nipashe TESA

Jumanne Juni 21, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Baada ya ruzuku ya petroli, dizeli

## • Ni zamu ya nishati za kupikia, gesi

KWANZA, namshukuru Mungu Mwenyezi kwa kuturehemu na kutujalia afya njema na mazingira ya amani ndani ya nchi hii.

Ni ukweli kuwa baada ya mafuta hasa petroli na dizeli kupanda bei wengi walipaza sauti wakilalamika kuwa maisha ni shida kwa mantiki kuwa bei za bidhaa zitaongezeka kutokana na gharama za usafirishaji.

Jambo hilo ni kweli kwani sembe sasa inaelekea Shilingi 1,800 kwa kilo wakati mafuta ya kula lita inaanzia Shilingi 8,000, huku sabuni mche ukiuzwa Shilingi 4,000 na sehemu nyingine za Jiji la Dar es Salaam nauli ya daladala inaelekea Shilingi 1,000.

Mathalani, mazao ya chakula kutoka mikoani mfano Kagera, Katavi, Kigoma, Ruvuma, Rukwa, au Tabora hadi Dar-es-Salaam gharama ya kuyasafirisha iliongeza bei kwa mlaji wa mwisho.

Siyo siku nyingi kulikuwapo na malalamiko kuhusu bei ya mafuta ya kupikia likajitokeza hili la ongezeko ya bei ya petroli na dizeli kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa serikali.

Kwa usikivu wa viongozi baada ya kuona sasa hali inazidi kuwa mbaya, ikachukua hatua na kuweka ruzuku kwa bidhaa za etroli.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ambayo, pengine Watanzania walitarajia kuona bei za mafuta zikishuka na kuleta unafuu.

"Serikali ilitoa ruzuku ya Shilingi bilioni 100 kwa petroli na dizeli pekee katika bandari zote tatu za Dar-Es-Salaam, Mtwara na Tanga kuanzia Juni 1, mwaka huu kwa kipindi cha mwezi mmoja". Kutokana na hatua hiyo bei ya mafuta ikashuka hivyo kupunguza, kwa kiasi fulani, gharama za usafirishaji."

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani Bukoba mkoa wa Kagera alitangaza rasmi kwamba ruzuku hiyo itakuwa ikitolewa kila mwezi mpaka bei za mafuta zitakapotengemaa. Anasema hiyo ni hatua mahususi ya serikali inayojali maslahi ya wananchi wake hivyo ni jambo la kupongeza na la kutia moyo.

Hata hivyo, mafuta yanapoagizwa kutoka nje ni pamoja na mafuta ya taa na gesi ya mitungi (LPG) ambayo ni bidhaa muhimu kwa matumizi ya nyumbani hususani kupikia chakula na kuwasha taa au vibatari kwa wasiokuwa na umeme wala nishati jua.



Kutumia mkaa na kuni ni kitisho kinachoelekea kuigeuza Tanzania jangwa. Iwapo gesi na umeme pamoja na vifaa vya kupikia vitapata ruzuku kama dizeli na petroli Watanzania wengi wanaweza kupunguza utegemezi wa mkaa na kuni jikoni. **PICHA: ZOTE MTANDAO**

### BEI MAFUTA YA TAA?

Baada ya serikali kutoa ruzuku na bei za mafuta zikashuka kidogo, vituo vya mafuta jijini Dar-Es-Salaam na kwingineko, vilishusha bei ya petroli ikipungua Shilingi 306 na dizeli 320 kwa lita moja tofauti na awali. Mhudumu alipoulizwa vipi mafuta ya taa ni kiasi gani akajibu, "hapa hatuuzi mafuta ya taa katafute sehemu nyingine".

Anapouliza kwa nini hayauzwi, anajibu:"Hayana faida tuliweka lita 10,000 tukakaa nazo miezi minne, tukaona biashara hiyo haifai tukaacha". Anaongeza: "Tumeweka nguvu kwenye biashara ya kuuza gesi, kidogo inalipa".

EWURA, inapoulizwa kuhusu mafuta ya taa, msemaji wake, Titus Kaguo, anaeleza kuwa huko nyuma kulishamiri uchakachuaji wa mafuta ya taa na kwamba kabla ya udhibiti wa hali hiyo matumizi yalikuwa lita 650,000 kwa siku.

Lakini, baada ya kuchukua hatua kudhibiti uchakachuaji kupitia mradi wa vinasaba, matumizi ya mafuta ya taa yakashuka hadi lita 90,000 kwa siku.

Vilevile, maalezo ya EWURA yanaonyesha kushuka kwa matumizi ya mafuta ya taa huko vijijini kutokana na juhudi za serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kufikisha umeme vijijini.

Pamoja na maelezo yake mafuta ya taa hayamo kwenye mpango wa ruzuku wakati bei yake ni wastani wa takribani Shilingi 3,300 kwa lita.

Licha ya REA kusambaza umeme vijijini siyo kila kijiji au kaya imepata umeme, lakini bei kubwa hiyo ya mafuta inapelekea wengi kutomudu matumizi yake.

### GESI VIJIJINI

Kwa upande fulani matumizi ya gesi yamekuwa yakiongezeka kutoka tani 10 mwaka 2006 hadi tani 200,000 mwaka 2021. Kwa vijijini kuna habari njema, gesi imeanza kutumika, kwa baadhi ya maeneo, yaliyotembelewa katika ziara iliyofanyika mwaka 2021 katika mikoa ya Katavi na Tabora.

Sehemu hizo kulikuwa na usambazaji wa gesi kwa kutumia mitungi midogo ya kilo tatu ingawa bado siyo wengi wanaotumia nishati hiyo, lakini huenda idadi ikaongezeka.

Watumiaji wanasema ni kwa upishi mwepesi kama kuchemshia maji, chai na kupika vyakula visivyohitaji muda mrefu kupikwa kama mboga, ugali na uji lakini si kwa maharage au makande.

Hivyo bado matumizi ya kuni ni makubwa mno na wachache sana kutumia mkaa vijijini na sasa changamoto kubwa kwa nishati za kupikia ni bei za gesi na mkaa pamoja na usambazaji wake.

### RUZUKU YA GESI

Matumizi ya umeme kupikia siyo makubwa kwa sababu ya gharama za umeme wenyewe na vifaa au majiko ya kuutumia kupika havishikiki.

Kama serikali imetoa ruzuku kwa petroli na dizeli vipi kuhusu

INAENDELEA UK.14

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU, KIGALI

# Australia yaikunjulia Tanzania mikono kuwa mshirika TEHAMA



Australia kusaidia kufanikisha masuala ya TEHAMA yanayohusisha mafunzo vyuoni UDOM, UDSM na DIT. **PICHA: MIRADJI MSALA**

MKUTANO Mkuu wa Maendeleo ya Mawasiliano Duniani (ITU WTDC - 2022), ukifanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika, umeipa Tanzania tumaini jipya kwenye sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ukilimalizika Rwanda mwishoni mwa wiki iliyopita mkutano huo unaoandaliwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (ITU), umejadili na kuweka mipango ya kuendeleza sekta ya mawasiliano duniani ikiangalia pia Afrika.

Mkutano huo unaiachia alama Afrika kwa kulenga kuweka mikakati ya kufanikisha jamii zote duniani zinaunganishwa kwenye mifumo ya mawasiliano.

Ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo unakutana na washiriki kutoka Australia kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Biashara ya nchi hiyo, katika mazungumzo, unaahidi kuiunga mkono kwa kuipigia kura ili Tanzania iwe mjumbe wa Baraza la Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa -ITU.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dk. Jabiri Bakari, akizungumzia mafanikio hayo, anawaambia wanahabari kuwa mazungumzo hayo yaliyofanyika pembezoni mwa ITU WTDC - 2022, yameleta tija kwa kuwa Australia imekubali kuiunga mkono Tanzania kwenye TEHAMA.

> “Ushiriki wa Tanzania kama mjumbe wa Baraza la ITU utaiwezesha kusimamia masuala muhimu ya kukuza uchumi wa kidijitali.

“Kiufupi tumekubaliana kushirikiana na Australia kwenye masuala ya kiufundi hasa eneo lote la TEHAMA likihusisha usalama mtandaoni. Aidha, imesema imevutiwa na uwepo wa vyuo vikuu vitatu vya Dodoma (UDOM) Dar es Salaam -UDSM na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam -DIT. Inaahidi kuendeleza mashirikiano na taasisi za elimu ya juu nchini,” anabainisha Dk. Bakari.

Anasema Idara ya Maendeleo ya Mawasiliano (BDT), ya ITU ndiyo inayoandaa Kongamano la Dunia la Maendeleo ya Mawasiliano (WTDC) kila baada ya miaka minne ili kupokea mada mbalimbali, kujadili utekelezaji na uanzishwaji wa miradi na programu muhimu kwa maendeleo ya mawasiliano duniani na kuangazia ukuaji wa sekta ya mawasiliano.

Aidha, anaeleza kuwa ITU WTDC - 2022 ni chombo cha juu zaidi cha kutunga sera cha ITU ambacho pia hupitisha mipango ya kimkakati na kifedha ya miaka minne na kuchagua timu ya wasimamizi wakuu wa shirika, nchi wanachama wa baraza na wanachama wa bodi mbalimbali za shirika hilo.

Anasema ikiwa ni mwanachama hai na mshiriki wa mkutano huo, Tanzania itatumia fursa hiyo kuomba kuungwa mkono kutoka nchi wanachama wa ITU ili kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la ITU kwenye mkutano mkuu wa shirika hilo utakaofanyika Bucharest nchini Romania, Septemba mwaka huu.

### UBORESHAJI MAWASILIANO

Dokta Bakari akizungumzia vipaumbele vya mdhibiti wa huduma za mawasiliano nchini, anasema TCRA imejizatiti kuwa mshiriki anayekwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia kwa kushirikiana na nchi zingine duniani kupokea na kuyatekeleza mageuzi ya TEHAMA.

“Matarajio yetu ni kuona mkutano huu unaiwezesha TCRA kuelewa upi hasa ni mwelekeo wa sekta ya mawasiliano na TEHAMA katika ujumla wake duniani ili tusiachwe nyuma; ushiriki wetu unaipa mamlaka nguvu ya kuwa mshiriki thabiti kwenye mabadiliko mbalimbali ya kiteknolojia duniani,” anafafanua Dk. Bakari.

Anasema kwenye mkutano huo wa Septemba, Tanzania itaomba kuchaguliwa kuwa miongoni mwa nchi wanachama wa Baraza la ITU, ikizingatiwa kuwa imekuwa kitovu cha kuziunganisha nchi zilizo mbali na ufuo wa Bahari ya Hindi kwenye mkongo wa mawasiliano wa baharini.

Anasema ujumbe kwenye baraza hilo utamaanisha kutetea maslahi ya ukanda wa Afrika hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara katika masuala ya ukuzaji TEHAMA.

Tanzania inaziunganisha Uganda, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Malawi na Kenya na mkakati ni kuendelea kusambaza huduma za Mkongo wa Mawasiliano hadi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Meneja wa Sehemu ya Usimamizi wa Rasilimali za Mawasiliano na Teknolojia wa TCRA, Mwesiga Felician, anabainisha kuwa Tanzania inashiriki katika kutoa maazimio mbalimbali ya sekta ya mawasiliano duniani.

“Tanzania imekuwa nchi yenye ushawishi wa TEHAMA kwenye ukanda wetu, lengo letu ni kutumia fursa ya mkutano huu kujinadi ili tuingie kwa mara nyingine kuwa mjumbe wa Baraza la ITU wakati wa Septemba mwaka huu kwani hii ni fursa ya kuongeza ushawishi wetu katika kukuza TEHAMA katika ukanda huu wa Afrika,” anabainisha Felician.

Anasema ushiriki wa Tanzania kama mjumbe wa Baraza la ITU utaiwezesha kusimamia masuala muhimu ya kukuza uchumi wa kidijitali.

Anasema ITU husimamia sekta tatu ikiwamo ya viwango, sekta ya maendeleo ya TEHAMA na sekta ya masafa.

Anasema ITU WTDC - 2022 ulitanguliwa na kongamano la mtandao wa vijana lililofanyika Juni 2 hadi 4 mwaka huu jijini Kigali, kujadili masuala mtambuka ya sekta mbalimbali za uchumi na namna TEHAMA inavyoweza kuchangia ukuaji wa uchumi kupitia sekta hizo.

“Tanzania ilishiriki kikamilifu kupitia TCRA na ujumbe wa vijana waliojikita katika fani za TEHAMA kutoka taasisi za elimu ya juu.”

Ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo unaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonaz na Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta Dk. Emmanuel Mannaseh anayeongoza washiriki kutoka TCRA.

TCRA inashiriki kama msimamizi mkuu wa sekta ya mawasiliano na wawakilishi wengine ni kutoka taasisi za elimu ya juu ambazo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha St. Joseph cha jijini Dar es Salaam.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA



Dereva Edmund Kinubi akiwa kazini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# M-Mama inavyomweka 'rahani' mjamzito, mtoto

MFUMO wa kielektroniki wa kitaifa wa kusafirisha kwa dharura wajawazito na watoto wachanga M-Mama, unaotumiwa zaidi vijijini, umethibitisha kuwa ni mwarobaini wa kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

M-Mama unaotumiwa kuwawahisha wajawazito kwenye huduma za kiafya ili kujifungua salama, unaelezwa kuwa umeokoa maisha ya mama na watoto wengi hapa Shinyanga, anasema dereva Edmundi Kinubi.

Ni dereva anayetoa huduma katika mahojiano na Nipashe, anasema hutolewa na madereva wa magari binafsi waliko vijijini wanaowapa msaada wa dharura muda wote mjamzito kwa kumtoa nyumbani na kumpeleka kwenye huduma za afya ili kujifungua salama.

Anaeleza kuwa ilianzishwa baada ya kuwepo changamoto ya usafiri kwa kinamama wajawazito hasa vijijini, ili kuwasaidia kwenda hospitalini badala ya kujifungulia njia au majumbani jambo linalosababisha ongezeko la vifo vinavyotokana na uzazi.

Kinubi anakumbusha kuwa mkoani Shinyanga, huduma ilianza mwaka 2017 kwa ushirikiano na kampuni ya Vodacom Tanzania Foundation, Vodafone Foundation na Shirika la Pathfinder International, lakini sasa ipo chini ya serikali.

Kinubi anayetoa huduma hiyo akisafirisha wajawazito kwa dharura kutoka nyumbani kwenda kwenye vituo vya afya, anajisifu kuwa ameokoa maisha ya wajawazito wengi.

Anasema ili kumfikia mama anapigiwa simu kwa namba za bure ambazo zimetolewa na Vodacom hivyo kuwahi kwa wakati ili kumfikisha mjamzito hospitalini haraka iwezekanavyo ili kujifungua salama.

Anasema tangu alipoanza kutoa huduma hiyo ya usafiri wa dharura kwa wajawazito mwaka 2019, ameokoa wajawazito wengi na kubainisha kuwa endapo asingewafikia huenda wangepoteza maisha kwasababu ya kukosa usafiri.

"Nakumbuka nimekumbana na matukio mengi kwa kuwakuta wajawazito katika hali mbaya, na baada ya kuwafikisha hospitalini walijifungua papo hapo,"anasema Kinubi.

"Kuna mwingine nilipomfikisha hospitali alijifungua lakini alipoteza damu sana, mfano huyu angejifungulia nyumbani ingekuwaje? Maisha yangeweza kupotea," anaongeza.

Anasema maeneo mengi ya vijijini hakuna usafiri salama kwa ajili ya wajawazito na huduma zake za afya hua zipo umbali mrefu, na mara nyingi usafiri ambao hutumia ni bodaboda au mikokoteni ya ng'ombe, ambayo hukatisha tamaa wajawazito na kuamua kujifungulia nyumbani licha ya kwamba ni eneo ambalo siyo salama.

Anasema kutokana na kufahamu tatizo hilo la ukosefu wa usafiri maeneo hayo ya vijijini, alikuwa anahakikisha gari lake linakuwa zima, lina mafuta ya kutosha, na simu yake kuwapo hewani wakati wote, ili akipewa taarifa anakuwa tayari kwenda kumchukua mjamzito na kumwahisha hospitali.

"Zamani nilikuwa nafanya biashara ya kusafirisha abiria wakati nikiendelea na huduma hii ya M-Mama ya usafirishaji wajawazito kwa dharura, lakini baada ya kuona wajawazito wengi wapo katika hatari ya kupoteza maisha, nikasitisha biashara ya kusafirisha abiria na kubaki kutoa huduma hii hadi sasa,"anaeleza Kinubi.

"Huduma hii ya kusafirisha wajawazito inataka moyo wa huruma pamoja na kujitoa sana, hapa Tinde tulikuwa madereva sita ambao tunatoa huduma hii, lakini wengine wote wameacha na kubaki peke yangu, sababu nimeguswa na wajawazito wanavyoteseka kwa kukosa usafiri, na kubebwa kwenye bodaboda na mikokoteni ya ng'ombe ni usafiri ambao siyo salama kwao," anasema Kinubi.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuzindua huduma hii ya M-Mama nchi nzima, ninachokiomba tu kwa serikali iboreshe miundombinu ya barabara hasa vijijini, ni kwa sababu kuna muda unashindwa kabisa kumfuata mjamzito nyumbani kwake, hadi asogezwe na bodaboda kuvuka upande wa pili ndipo upakie kwenye gari na kuwahi hospitali. Hili si jambo jema anaweza kuchelewa . Kama barabara zingefunguka ingekuwa rahisi zaidi kumsaidia," anaeleza Kinubi.

Mnufaika wa huduma hiyo ya M-Mama ya usafiri wa wajawazito kwa dharura, Judith Kayegeji, anasema bila kuwapo na huduma hiyo huenda angekuwa ameshapoteza maisha.

Anasema ilimnusuru kwa kumuwahisha hospitali na alipojifungua alipoteza damu nyingi, lakini kutokana na huduma na wataalamu yeye na mtoto wake wako salama.

Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Flora Kajumulla, anasema huduma hiyo ya M-Mama, imekuwa msaada mkubwa mkoani humo na imepunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

> Vifo vya watoto wachanga mwaka 2016 vilikuwa 1,080, lakini mwaka jana 2021, kutokana na M-Mama vimepungua hadi 665 sawa na asilimia 45.

Anasema huduma hiyo kwa sasa inasimamiwa na serikali na kwamba madereva wanaowahudumia wajawazito huwalipa, na kila wanapombeba mjamzito na kumfikisha kwenye huduma ya afya kuna kuna fomu za kujaza na mwisho wa mwezi hulipwa pesa zao.

Anasema tangu huduma hiyo ya M-Mama ianze kufanya kazi mkoani Shinyanga mwaka 2017, hadi kufika mwaka jana imeshawafikia kinamama 5,769.

Wamepatiwa elimu ya afya ya uzazi pamoja na kuhimizwa kujifungulia kwenye huduma za afya maeneo ambayo ni salama.

"Mwaka 2016 vifo vya mama vitokanavyo na uzazi vilikuwa 74, lakini baada ya kuanza huduma hii ya M-Mama mwaka 2017 na hadi kufikia mwaka jana (2021) tulipunguza vifo hadi 50 sawa na upungufu wa asilimia 40," anasema Kajumulla.

"Vifo vya watoto wachanga mwaka 2016 vilikuwa 1,080, lakini mwaka jana 2021, kutokana na M-Mama vimepungua hadi 665 sawa na asilimia 45," anaongeza.

# Baada ya ruzuku ya petroli, dizeli

INATOKA UK.11

gesi na umeme ili kuwezesha wakazi wengi mijini kutumia badala ya mkaa na kuni?

Iko haja kwa serikali kulitazama jambo hili ili kuleta ahueni kwa matumizi ya gesi ya mitungi LPG na umeme kupikia kama ilivofanyika kwa wasafirishaji wanaotumia dizeli na petroli.

Serikali ikifanya hivyo itapunguza matumizi makubwa ya mkaa na kuni nchini, hivyo kuimarisha ubora wa mazingira nchini na kufikia lengo la kulinda misitu ya asili ili istawi ipasavyo na taifa kunufaika na huduma za kiikolojia zitokanazo na uwepo wa misitu iliyo na afya nzuri hadi kusababisha kupunguza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi, yanayoongeza joto duniani.

Nithubutu kueleza kwamba Wizara ya Nishati tangu uhuru haijaweka mkazo katika sera zake kuhusu nishati ya kupikia. Mfamo, kuwepo kifungu cha bajeti kuhusu nishati ya kupikia na kutengewa fedha za kutosheleza mahitaji.

Kwa miaka kadhaa sasa mkazo umewekwa katika matumizi gesi asilia kuzalisha umeme. Kwa upande wa nishati ya kupikia nchi imeegemea zaidi kwenye misitu kupata kuni na mkaa.

Lakini, uwezo wa kuisimamia misitu umekuwa siyo wa kuridhisha na matumizi ya mkaa na kuni yameshamiri kiasi cha serikali au Wizara ya Nishati kutohangaikia kupata nishati mbadala na endelevu.



Majiko ya umeme na gesi ni mbadala wa kuni na mkaa. **PICHA: MTANDAO**

Ingekuwa serikali imeweka mkazo kwa usimamizi wa misitu kiasi kwamba hata mkaa utokane na misitu iliyosimamiwa kikamilifu ukataji miti kwa kuni na mkaa ungedhibitiwa na mkaa usingezagaa ovyo mitaani.

Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Idara ya Misitu na Nyuki jukumu lake ni kuilinda na kuisimamia misitu ya asili ili huduma na bidhaa zitokanazo na rasilimali misitu zipatikane kwa misingi ya matumizi endelevu sasa hali siyo hivyo.

Misitu mingi inatumika kwa matumizi yasiyoendelevu, watu wanaingia na hutengeneza mkaa wanavyotaka.

Udhibiti wake ni mdogo sana ni "mashamba ya bibi" na madhara yake ni uharibifu mkubwa wa mazingira. Iwapo taifa litarejea kwenye misingi ya taaluma kuhakikisha upatikanaji mkaa unatokana na misitu inayosimamiwa ipasavyo, Watanzania watahifadhi mazingira.

Hapa ndipo serikali inatakiwa kuchukua hatua ili kupunguza bei za gesi/LPG na umeme pamoja na vifaa vya kutumia ili familia nyingi ziachane na mkaa.

Hatua hiyo itasaidia kuokoa misitu isiendelee kuharibika na kuigeuza Tanzania kuwa jangwa.

Aidha, ni tija kwa kuwa wakulima watazalisha mazao zaidi ya kilimo, kupata asali zaidi, kupunguza mmomonyoko wa udongo kwa kuongeza uoto wa asili na pia kupunguza gesiukaa ($CO_2$) angani na kuongeza mchango wa misitu kwa sekta za mazingira. Kadhalika ili kuwa na uhakika wa maji baharni, mitoni na maziwani, kuwa na mvua ya kutosha, kilimo, mifugo, umwagiliaji, utalii, afya, elimu, makazi ya wanyamapori.

Hili ni ombi langu na wana mazingira kwa serikali inayoongozwa na CCM ili bei za gesi ya mitungi-LPG, mafuta ya taa na umeme na vifaa vya kupikia kama majiko ya umeme yenye presha, mabirika ya kuchemshia maji na majiko yenye muunganiko wa umeme na gesi ili taifa lipunguze kutumia mkaa na kuni.

## WANENAVYO MALENGA

### WANAFAA KWA MSIMU

Wanafaa kwa msimu, hao ndio wanadamu,
Kwako wala hawadumu, hata usiwashutumu,
Ni sababu maalumu, kwako wanakuwa zamu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Tujuavyo wanadamu, wapenda vitu vitamu,
Uwenavyo wakushumu, uonekane mtamu,
Watapishana kwa zamu, kama keki siyo ndimu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Waone una kalamu, mwandiko waufahamu,
Watrema vitamutamu, mashavu yavikaimu,
Utakuwa ni mtamu, Mcharo hawana hamu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Mambo yaanze ugumu, bila wewe kufahamu,
Asubuhi ujihimu, uwaone binadamu,
Rafiki wengi ka timu, wale uliwahudumu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Wana akili timamu, na wewe wafahamu,
Kama hawakufahamu, watakupita kwa zamu,
Wako bize wafahamu, nawe hawakufahamu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Kabila la wanadamu, wewe kwao ni muhimu,
Kwa yao mambo muhimu, hapo watakufahamu,
Ukiwatolea sumu, tabaki wawalaumu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Wapigika piga simu, kupokea alaumu,
Umekwishakuwa sumu, ingawa uliwakimu,
Umeshapewa hukumu, huwafai mwanadamu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Mungu peke anadumu, atufaa wanadamu,
Milele siyo kwa zamu, mapenzi yake adhimu,
Huko bora unda timu, kwa amani ya kudumu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

Tujifunze wanadamu, pendo lile la kudumu,
Tufaidipo matamu, nasi tuwe binadamu,
Tusijigeuze sumu, kule tunakojikimu,
Tunaye Mungu pekee, afaa kwa kila kitu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### TENDA WEMA UONDOKE

Katika maisha yako, hebu chunguza chunguza,
Ufanyapo kazi zako, kwa Mungu wako penyeza,
Kwa huo uwezo wako, umpendeze Muweza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Katika eneo lako, macho unavyoangaza,
Ndugu na jirani zako, unapowaona waza,
Kama kwa nafasi yako kusaidia waweza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Unaona njaa iko, shilingi yako penyeza,
Wakila furaha yako, na kwa Mungu yapendeza,
Na tena kwa tendo lako, wala si kujitangaza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Hizo jitihada zako, ongeza nakuhimiza,
Hiyo ni sadaka yako, si kazi ya kuchombeza,
Hiyo ni akiba yako, anaitunza Muweza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Unao watoto wako, shule wawaendeleza,
Ila kwa jirani zako, watoto wachezacheza,
Hizo jitihada zako, hata huko endeleza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Kama kwa mkono wako, kufanyafanya waweza,
Hao majirani zako, maisha wakayaweza,
Hiyo ni baraka kwako, kwa Mungu inapendeza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Maisha yako si yako, zidi kuyaendeleza,
Mtoto wake ni wako, mwendeleze ukiweza,
Huijui kesho yako, kukutunza anaweza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Kuna wengi watu wako, wala si wa kujikuza,
Wapenda huku na huko, bila ulizauliza,
Mungu aonaye yuko, afurahi awakuza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

Ndugu nakupa mwaliko, mali kakupa Muweza,
Kwako liwe changamko, kwa wengine kusambaza,
Sitegemee mshiko, ili uweze koleza,
Tenda wema uondoke, kwa Mungu hiyo sadaka.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



# CCM yampongeza Samia kutoa bil.373/- za miradi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ya kuiongoza serikali, kutenga Sh. bilioni 372 kwa ajili ya kutekeleza miradi maendeleo katika mkoani Dodoma.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, akisoma tamko hilo juzi alisema wanaishukuru serikali kwa kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya 2022/2023 kwa ajili ya barabara za mzunguko, Uwanja wa Ndege wa Msalato na ukamilishaji wa Ikulu ya Chamwino.

"Katika bajeti kuu ya serikali iliyosomwa Juni 6, mwaka huu yenye jumla ya Sh. trilioni 41.5 Mkoa wa Dodoma umetengewa kiasi cha Sh. bilioni 372 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni Sh. bilioni 126.8 na Sh. bilioni 245 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida,"alisema.

Mkanwa alisema CCM Mkoa wa Dodoma itaendelea kusimamia matumizi mazuri ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa mkoa, ikiwamo utolewaji wa mikopo, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani, kusimamia ujenzi wa zahanati 40, vituo vya afya 21 na hospitali za wilaya sita.

Mkanwa alisema bajeti iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, bungeni imejielekeza kumkomboa mwananchi wa kawaida kiuchumi, kisasa na kijamii katika sekta ya elimu, afya na kilimo.

"Bajeti hii imeeleza kuwa kuanzia mwaka wa fedha ujao mtoto wa kitanzania atapata elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita, pia kupitia Wizara ya Kilimo mkulima wa kawaida atapata ahueni ya bei ya chini ya pembejeo bora msaada wa kitaalamu.

"Sisi tunasema Mwenyekiti wa CCM ambaye ni Rais wa Tanzania, Samia ameupiga mwingi kwa jitihada zake za kutangaza vivutio vya utalii kupitia filamu ya The Royal Tour ambayo imefungulia ongezeko la watalii nchini.

Aliongeza kuwa wanamshukuru Rais Samia kwa kuongeza mshahara kwa asilimia 23, nyongeza ya posho za safari, kutoa vibali vya ajira mpya na kuendelea kusimamia vizuri rasilimali za Taifa.



Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Mbaga, alisema katika kuhakikisha wanajitegemea kiuchumi wamejenga fremu za kupangisha 174, kwamba wanatarajia kukusanya zaidi ya Sh. bilioni moja kwa mwaka.

Alisema ujenzi wa mradi huo upo katika hatua ya kukamilika na unatarajia kumalizika ifikapo mwishoni mwa mwezi huu na umegharimu Sh. milioni 890.

"Fremu zote zimepata wateja na kodi ya mwezi ni Sh.500,000 na kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kulipa mishahara ya watumishi na posho. Tunataka mkoa wetu uwe wa mfano na wajumbe wengine waje kujifunza kwetu na hadi sasa sisi ndiyo tunaongoza," alisema.

Mbaga aliwataka viongozi wa CCM ngazi ya wilaya kuhakikisha wanajielekeza katika miradi ya kimkakati ili waweze kujitegemea kiuchumi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania (UWT) Mkoa wa Dodoma, Neema Majule, alisema lengo la kuanzisha miradi hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha CCM inajitegemea kiuchumi na kuepuka kuwa omba omba.

## Askofu aomba wenye matatizo ya akili wahesabiwe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Shilo Ministries of Tanzania, Richard Ruta, ameiomba serikali kutowasahau watu wenye matatizo ya afya ya akili wakati wa Sensa ya Watu na Makazi.

Alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya kanisa hilo kuhusu maandalizi ya sensa kwa mwaka huu.

Kiongozi huyo wa kanisa aliiomba serikali kwenye uandikishaji wa sensa watu wenye matatizo ya afya ya akili wasisaulike kwenye kuhesabiwa kwa kuwa na wao wana haki sawa na wengine.

Kadhalika, aliiomba serikali kutumia njia mbalimbali zitakazowezesha watu hao kuhesabiwa hata kama hali zao siyo nzuri.

"Pamoja na kuwa tunafahamu baadhi yao afya ya akili haiko vizuri na wengine wanaishi kwenye maeneo hatarishi na yasiyo rasmi, tunaiomba serikali isiwasahau na kuwabeza, bali wanatakiwa kuhesabiwa kama ilivyo kwa watu wengine,"alisema.

Pia aliziomba familia zenye watu wenye ulemavu kuwa na ushirikiano na serikali katika kutoa takwimu sahihi za watu wanaoishi nao ili zoezi hilo lifanikiwe kwa wakati na uaminifu.

Askofu Ruta alisema sensa ya watu na makazi ina faida kwa kuwa serikali itaweza kupanga mipango yake vizuri ya bajeti kwa ajili ya watu wake, hivyo wananchi wawe tayari kutoa ushirikiano.

Hata hivyo aliwataka Watanzania kuombea zoezi hilo ili lifanyike kwa mafanikio na kuiwezesgha serikali kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kutekeleza na kupanga bajeti kulingana na mahitaji ya wananchi.




Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende, akikata utepe kwa ajili ya makabidhiano ya nyaraka za ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inayotarajiwa kujengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Kulia ni Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Devotha Ngulugulu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DUWASA yataja sababu za mgao wa maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, amesema kwa sasa mahitaji ya maji katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 133 kwa siku.

Amesema uzalishaji ni lita milioni 67 hali inayosababisha kuwapo kwa mgao wa maji. Mhandisi Joseph, alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa uwekezaji na maendeleo ya sekta ya maji.

Alisema kwa sasa mahitaji ya maji katika Jiji la Dodoma ni lita milioni 133 kwa siku, wakati uzalishaji ni lita milioni 67 kwa siku hali inayosababisha kuwapo na mgao wa maji.

Kadhalika, alisema kutokana na hali hiyo mamlaka inampango wa kuchimba visima maeneo ya pembezoni ya Jiji ikiwamo Nala na Ntyuka, ili kupunguza utegemezi katika chanzo cha Bonde la Makutopora (Mzakwe).

Alisema hatua nyingine ya kukabiliana na mgao huo ni mpango wa utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Bwawa la Mtera, ujenzi wa Bwawa la Farkwa pamoja na Ziwa Victoria. Akizungumzia kuhusu usafi wa mazingira, alisema mamlaka hiyo hivi sasa inatekeleza mradi mkubwa wa ukarabati wa mtandao wa majitaka maeneo ya Area C na D urefu wa kilomita 19 kwa Sh. bilioni 4.9.

"Pia tunatekeleza mradi mpya mkubwa wa mtandao wa majitaka katika Jiji la Dodoma wa dola za Marekani milioni 70, ambazo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim-India na takribani kata 11 zitafikiwa,"alisema Joseph.

Alisema usomaji wa mita za maji hivi sasa ni shirikishi kupitia ujumbe mfupi wa maneno unaotumwa kwa mteja na kuwataka wateja wazingatie jumbe hizo ili kuepuka malalamiko ya kubambikiwa bili za maji.

Vilevile, aliwata wateja waendelee kutoa taarifa kupitia majukwaa mbalimbali ya DUWASA kama makundi sogozi, mitandao ya kijamii na namba ya simu ya bure ambayo ni 0800110078.

Aidha, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipa Dodoma kipaumbele kwa kuipatia fedha ya kuwezesha kutekeleza miradi ya hati ya dharura.





# 'Asilimia kubwa magari ya shule ni mabovu'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA kubwa ya magari ya shule mkoani Mbeya yamebainika kuwa mabovu kwenye mifumo mbalimbali ikiwamo breki hali inayohatarisha maisha ya wanafunzi wanaoyatumia kwenda shuleni na kurejea nyumbani.

Hali hiyo ilibainika mwishoni mwa wiki wakati Jeshi la Polisi mkoani humo Kikosi cha Usalama Barabarani lilipofanya ukaguzi maalumu wa mabasi hayo katika Kituo cha Ukaguzi wa magari cha Nanenane jijini hapa. Ukaguzi huo ulifanywa na wataalamu wa mifumo ya magari wakiongozwa na Mkuu wa Kikosi hicho, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Meloe Buzema, alisema zoezi hilo lilikuwa maalumu kwa ajili ya kuangalia usalama wa magari hayo.

Alisema baadhi ya magari hayo yalikuwa na matatizo ya ubovu wa mifumo ya breki ambayo baadhi yake mifumo hiyo imepasuka na inaweza kuachia muda wowote na kusababisha madhara kwa wanafunzi pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

Alisema magari mengine yalibainika kuwa na matatizo kwenye mifumo ya usukani hali ambayo pia inaweza ikahatarisha maisha ya wanafunzi endapo yataachwa yaendelee kufanya kazi.

"Tutaziondoa namba za magari haya ili yasifanye kazi tena barabarani mpaka watakapoyafanyia matengenezo, watakwenda kuyatengeneza na wakimaliza watayaleta kwa ajili ya ukaguzi wa mara ya pili na kama yataonekana yako vizuri wataruhusiwa kuendelea na kazi, lakini kama yatakuwa bado yana matatizo tutayazuia," alisema Buzema.

Baadhi ya madereva waliokuwa wanaendesha magari hayo walikiri kuwa yana matatizo na wakaeleza kuwa wao wamekuwa wakitimiza wajibu wao wa kuwaeleza wamiliki, lakini utekelezaji wa matengenezo ndiyo tatizo.

Mmoja wa madereva hao, Atupele Lazaro, alisema ukaguzi huo uliofanywa na Jeshi la Polisi ni mzuri na ulikuwa na lengo la kuwakumbusha kuhusu kuyafanyia matengenezo ya mara kwa mara magari yao.

Alisema mbali na kuwakumbusha, lakini ukaguzi huo unasaidia kuokoa maisha ya wanafunzi pamoja na madereva wenyewe wanaoendesha magari hayo kwa maelezo kuwa yakipata ajali hata wao wanadhulika.

"Huu utaratibu ni mzuri sana, tunaomba ikiwezekana uwe endelevu maana unatusaidia kuwakumbusha hata matajiri wetu ambao ndio wenye majukumu ya kutoa bajeti ya matengenezo," alisema Atupele.

Naye Frank Sanga alisema, wakati mwingine hata dereva anaweza akajisahau kumweleza mmiliki kuhusu matatizo ya gari jambo ambalo bila kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara inakuwa vigumu magari hayo kurekebishwa.

Alisema wapo baadhi ya wamiliki wa magari hayo pia ni wagumu kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo na kuliomba jeshi hilo kuendelea kutoa elimu ya usalama barabarani. Katika hatua nyingine Kamanda Buzema alisema jeshi hilo linamshikilia dereva wa gari la Kampuni ya Arusha Express linalofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Arusha, Mussa Issa, kwa kosa la kuendesha basi akiwa amelewa kupindukia.

Kamanda Buzema alisema walifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye mabasi na kumkuta dereva huyo akiwa anaendesha huku amelewa na walipompima walibaini kuwa alikuwa na kilevi chenye ujazo wa miligramu 236.

Alisema hali hiyo ni hatari kwa usalama wa abiria na mali zao na kusisitiza kuwa wataendelea kufanya ukaguzi huo na dereva huyo atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Gaudentia Kabaka (kushoto), akimsikiliza mdau wa maendeleo wa mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alipokuwa anapokea nyumba ya jumuiya hiyo mkoani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Jumuiya CCM zatakiwa kubuni miradi maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUMUIYA za Chama Cha Mapinduzi (CCM), zimetakiwa kubuni miradi ya kuziingizia kipato ili ziondokane na utegemezi unaozifanya kupata viongozi wenye uwezo hafifu.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Gaudentia Kabaka, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya alipokuwa anaweka Jiwe la Msingi kwenye mradi wa nyumba za kupangisha wa UWT mkoani hapo.

Nyumba ya awali ya mradi huo imejengwa kwa msaada na mdau wa maendeleo Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela kwa gharama ya Sh. 7,000,000 kuanzia kwenye msingi mpaka kwenye hatua ya uwezekaji.

Kabaka alisema mradi huo wa UWT unatakiwa utumike kama wa mfano kwa jumuiya zingine na kuwashauri viongozi kwenye mikoa mingine kujifunza kupitia mradi unaotekelezwa mkoani humo.

Alimshukuru Mwaselela kwa kuisaidia jumuiya hiyo kutekeleza mradi huo na akawaomba wadau wengine kusaidia kukamilisha mradi huo hasa kwenye eneo la uwezekaji.

"Ndele ni mtu wa ajabu sana, anasaidia jumuiya hii sio kwamba anatafuta cheo kwenye hii jumuiya ila anasaidia kwa sababu ana upendo na kinamama, namshukuru sana kwa kusaidia mradi huu," alisema Kabaka.

Katibu wa UWT Mkoa wa Mbeya, Mary Mwasengo, alisema walianza kujenga nyumba hiyo kwa kuchangishana, lakini wakiwa kwenye moja ya mikutano ya harambee Mwaselela aliahidi kuwachangia Sh. milioni 10 kwa ajili ya mradi huo. Alisema mradi huo umefikia hatua ambayo wanahitaji kukamilisha na kuwaomba wadau wengine wawasaidie kukamilisha.

Akizungumza wakati wa kukabidhi nyumba hiyo, Mwaselela alisema awali aliahidi kutoa fedha, lakini baadaye akabaini kwamba zingeleta migogoro na kuamua kupeleka vifaa pamoja na kugharimia ufundi.

Alisema mpaka sasa ametumia zaidi ya Sh. milioni 7.5 na chenji iliyobaki anakusudia kuitumia kwa ajili ya kununua mbao za kuezekea nyumba hiyo.

Alisema pia, amekuwa akisaidia jumuiya hiyo kwa vitu vingine ikiwamo kusomesha watoto.

# 'Mzee wa Upako' awaondoa hofu wanachama

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Mbeya Mjini, John Mwambigija, maarufu kwa jina la 'Mzee wa Upako' amesema bado ni kiongozi wa chama hicho na kinachoendelea ni upepo wa kawaida.

Mwambigija pamoja na wajumbe wengine 11 wa Halmashauri Kuu ya Chama hicho, Wilaya ya Mbeya Mjini, waliondolewa kwenye nafasi zao na uongozi wa chama hicho Kanda ya Nyasa kutokana na kilichotajwa kuwa ni watovu wa nidhamu.

Viongozi hao waliondolewa mwezi Januari, mwaka huu na Mwenyekiti wa kanda hiyo, Mchungaji Peter Msigwa, alitangaza uamuzi huo na kuagiza uongozi wa chama hicho mkoa kuunda kamati ya muda ya kusimamia shughuli mpaka utaratibu mwingine utakapotangazwa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye Mkutano Mkuu wa CHADEMA, Wilaya ya Mbarali, Mwambigija alisema yeye pamoja na wenzake bado ni viongozi ndani ya chama hicho licha ya mizengwe inayoendelea.

"Sisi bado ni viongozi na tutaendelea kuwa viongozi ndani ya chama hiki, kinachotokea ni upepo wa kawaida unaopuliza matete ambayo yanayumba sana, lakini hayawezi kuanguka, kwahiyo tutaendelea kuchapa kazi," alisema Mwambigija.

Alisema binafsi anaendelea na harakati za kukijenga chama hicho kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya na kwa sasa wanaiomba serikali iruhusu mikutano ya siasa ili wafanye siasa za ushindani.

Aidha, Mwambigija aliiomba serikali kutumia busara kuwaondoa wafugaji wa Kimasai kwenye maeneo mbalimbali ya hifadhi za taifa badala ya kutumia nguvu akidai kuwa ni raia kama wengine wanaostahili kuhudumiwa vyema na serikali.

Alisema kwa muda mrefu wafugaji hao wanaishi vyema na wanyama hasa kwenye maeneo ya Bonde la Ngorongoro na Loliondo na hawajawahi kuhudhuriwa na wanyama na kuiomba serikali iendelee kuwaacha.

"Hawa jamaa wamekuwa wanawasaidia baadhi ya wanyama wanaopata shida kuzaa, lakini wamekuwa wakisaidia kuwakwamua wanyama wanaokwama kwenye tope na maeneo mengine jambo ambalo ni jema, sasa ni lazima tuwatetee," alisema Mwambigija.

Aliwabeza baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wanaofurahia serikali kuwaondoa wafugaji hao kwenye maeneo yao akidai kuwa watakuwa wamelambishwa asali 'rushwa'.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Msigwa, alisema baada ya serikali kuruhusu mikutano ya siasa watahakikisha wanafanya mikutano mingi ya kukijenga chama kwa wakati mmoja.

Alisema watakuwa wanatumia 'chopa' (ndege) kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine ili kufanya mikutano mingi na kwa haraka zaidi kwa ajili ya kukijenga chama.

Alisema chama hicho bado kina nguvu kubwa kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na ndiyo maana serikali inaogopa kuruhusu mikutano.



## Wananchi waelezwa umuhimu kudai risiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wananchi kufahamu umuhimu wa kukusanya kodi kwa kutumia mashine za kielektroniki ili kukuza pato la nchi.

Aliyasema hayo baada ya kumaliza matembezi ya kuhamasisha kampeni ya kudai risiti za kielektroniki yaliyoambatana na mazoezi ya viungo yaliyoanzia Ofisi za Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Mzizini na kumalizikia Uwanja wa Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Alisema ni vyema wananchi wakadai na kutoa risiti kwa wanaofanya miamala ya kibiashara ili kudhibiti ukusanyaji wa mapato yasipotee.

Hemed alieleza kuwa jukumu la msingi kwa serikali ni kuweka mipango madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ambayo yatatumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuijenga Zanzibar mpya.

Aliwataka Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufikisha elimu ya kudai na kupokea risiti kwa wananchi katika majimbo yao ili elimu hiyo iwafikie wananchi wote.

Hemed pia, aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa wasiodai na wasiotoa risiti ili kuwadhibiti wanaokiuka sheria hiyo na wanaouhujumu uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, alieleza kuwa ni vyema kwa wauzaji na wafanyabiashara kuweka matangazo katika maeneo yao ya biashara ambayo yataonyesha umuhimu wa kudai risiti kwa anayenunua bidhaa katika maeneo yao ya kazi.

Alisema wanamichezo wana ushawishi mkubwa katika jamii na Baraza la Wawakilishi limeamua kuandaa matemebezi hayo pamoja na mazoezi ya viungo ili kuamsha ari ya uelewa kwa jamii.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema wizara imejipanga kukusanya mapato katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwa wafanyabiashara na kuwaomba wananchi kuendelea kuunga mkono juhudi hizo kwa kudai risiti kwa anayefanya miamala.

Kwa upande wake, Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Yussuf Juma Mwenda, alisema suala la kulipa kodi ni la kila mmoja na serikali imejipanga kuongeza mapato yake kwa njia ya kisasa ili kuweka kumbukumbu kwa wanaofanya biashara.

# TASAF yakarabati shule aliyosoma baba Samia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF), umeifanyia ukarabati shule ya msingi na sekondari Piki, kisiwani Pemba ambayo aliwahi kusoma baba wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Shule hiyo iliyojengwa mwaka 1969, TASAF imeamua kuifanyia ukarabati huo baada ya wananchi kuomba kutokana na kuchakaa na kuhatarisha maisha ya wanafunzi na walimu.

Akizungumza na waandishi wa habari shuleni hapo, Katibu wa Kamati ya ujenzi huo, Rubea Muhammed Said, alisema kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza tatizo la uhaba wa madarasa na uharibifu wa mali za shule.

Alisema TASSAF imegharamia ukarabati wa madarasa na ujenzi wa uzio wa shule hiyo ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika kwa gharama ya Sh. milioni 328.

"Tunaishukuru sana TASAF kwa msaada wao kwa sababu mazingira ya shule yalikuwa mabaya sana kutokana na majengo haya kuwa ya muda mrefu na kuchakaa," alisema Rubea.

Alisema licha ya ujenzi huo wa shule, lakini wananchi wa kijiji cha Piki wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa kituo cha afya dna kulazimika kufuata matibabu kijiji jirani cha Mtabwe kilichoko masafa marefu.

Aliiomba TASAF na wadau wengine wenye uwezo kusaidia ujenzi wa kituo cha afya kijijini hapo ili kuwaondolea tatizo wanalokabiliana nalo hasa kwa wajawazito na watoto.

"Hatuna kituo cha afya hata wajawazito wanapochunguzwa afya zao zoezi hilo hufanyika pale kiwanja cha mpira wataalamu wa afya hufika hapo...hali hiyo haileti taswira nzuri," alisema.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Hassan Ali Muhammed, alisema uongozi wa shule umefurahishwa na ukarabati wa shule hiyo na utakapokamilika wanafunzi watapata elimu katika mazingira mazuri.

Alisema pia wanahitaji maabara na kitengo cha huduma ya kwanza ili wanafunzi wanapopata majeraha au kuugua ghafla wapate huduma kwa haraka.

Kwa upande wake Ofisa Mdhamini, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ali Salum Matar, alisema TASAF ni chombo maalum cha kutekeleza mipango ya maendeleo katika jamii ili kuondoa changamoto zinazowakabili.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha unaomaliza kuna miradi miwili imetekelezwa kisiwani Pemba ikiwamo kituo cha afya katika kijiji cha Kendwa kitakachokuwa mkombozi kwa vijiji mbalimbali na kupunguza kadhia ya wananchi wanaosafiri masafa marefu kufuata huduma za afya.

Alisema pia mradi wa ujenzi wa ukarabati wa Shule ya Piki utakuwa mkombozi kwa wanafunzi wa wananchi wa kijiji cha Piki.




Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman (watatu kushoto), akimlisha keki maalum Mwenyeki wa Bodi ya Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Ramadhani Mwalimu Khamis, ikiwa ni ishara ya kulipongeza shirika hilo kwa kutimiza miaka 53 tangu kuanzishwa kwake katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki visiwani humo. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mkuu wa ZIC, Arafat Haji (wapili kushoto), Naibu Kamishna Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Said (kulia) na Mkurugenzi wa Bima ya Kawaida wa ZIC, Jape Khamis. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZIC kusogezea wateja huduma kimtandao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Bima Zanzibar (ZIC) limehitimisha maadhimisho ya miaka 53 tangu kuanzishwa kwake kwa kuzindua programu ya mtandao (Online App) ijulikanayo ZIC App ikilenga kusogeza huduma zake karibu zaidi na wateja.

Uzinduzi wa programu hiyo ulifanyika visiwani humo wakati wa hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na shirika hilo kwa ajili ya wadau mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maadhimisho hayo na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman, alisema mafanikio hayo yanaashiria shirika hilo lipo imara kiutendaji na inaithibitishia serikali kuwa umefika muda muafaka kulipatia uhuru wa kujiendesha kiushindani ili kutengeneza faida zaidi. "Maendeleo haya makubwa tunayoyashuhudia yakiwamo ya kiteknolojia, yanatuongezea imani kwamba sasa umefika wakati tuwape uhuru zaidi ili kujiendesha kwa ushindani na kusimamia mambo yenu bila kuingiliwa wala kuhodhiwa sana na serikali," alisema.

Hata hivyo, alibainisha kuwa changamoto kubwa iliyo mbele ya shirika hilo ni kuhakikisha kuwa linasogeza zaidi huduma zake hadi vijijini kwenye idadi kubwa ya wananchi hususani wakulima, wavuvi na wafanyabiashara wadogo ambao hawajafikiwa na huduma hiyo.

"Ni dhamira ya serikali kuona huduma za kibima zinaelekezwa pia kwenye maeneo ya pembezoni ambako kuna wananchi wengi ambao nao wanaohitaji kupatiwa huduma za bima. Wananchi wengi wanapoteza mitaji na mazao yao katika maeneo mbalimbali kutokana na majanga mbalimbali hivyo ni matarajio ya serikali kuwa huduma zenu zitawagusa zaidi hao pia," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ZIC, Arafat Haji, alisema ukuaji wa shirika hilo unaoshuhudiwa kwa sasa ni matokeo ya ushirikiano baina yake na wadau wake wakiwamo wateja na washirika kibiashara likiwamo Shirika la Posta Tanzania ambao kupitia ushirikiano wao wamejitanua nchi nzima.

"Pamoja na yote hayo ni kwa muda mrefu sasa ZIC tumekuwa tukijikita zaidi kwenye uwekezaji wa mifumo ya kidigitali itakayotuwezesha kuwafikia wateja wengi zaidi, kwa urahisi zaidi, mahali popote walipo na hivyo kuwaondolea wateja wetu ulazima wa kutembelea matawi yetu pindi wanapohitaji huduma zetu...ujio wa ZIC App ndio kilele cha mafanikio hayo," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Said pamoja na kulipongeza shirika hilo kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 53, alitoa wito kwa kampuni ya bima nchini kuendelea kubuni zaidi huduma mbalimbali za kibima ili kuongeza wigo wa huduma za kibima na njia (distribution channels) za kuwafikia wateja wao.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 415 YA 2022**
**ABDALLAH MUSA KARADENGA (Minor)**
**ABDULKARIM MUSA KARADENGA (Minor)**
**LILIAN PETER HAULE (The Guardian)**
**…………………WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MUSA RASHIDI KARADENGA, STEPHANO KINKORO……MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA MUSA RASHIDI KARADENGA**
Popote ulipo Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe **21/06/2022** mbele ya Mwenyekiti M.Khasimu wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
**Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 31.05.2022.**

**M. KHASIM**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 418 YA 2022**
**ABDALLAH MUSA KARADENGA (Minor)**
**ABDULKARIM MUSA KARADENGA (Minor)**
**LILIAN PETER HAULE (The Guardian)**
**………………WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MUSA RASHIDI KARADENGA, STEPHANO KINKORO……MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA MUSA RASHIDI KARADENGA**
Popote ulipo Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe **21/06/2022** mbele ya Mwenyekiti M.Khasimu wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
**Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 31.05.2022.**

**M. KHASIM**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GADI HILARY MBWILO,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari , yenye namba za usajili **T 269BJY** Yenye Chassis namba **ZC115116297,** Engine namba **M13A1600150** Yeyote atakayeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**Polisi Taarifa : KIL/MOS/RB/568034/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU MUSSA ALLI LUPATU** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T635AHL** aina ya NISSAN SAFARI yenye Eng. **No.TD4205542** na **Chasis No. WRG100500222** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/240382/2022**

**Summons to appear (O.V.R.20 (1) (CPC)**
**(Substituted services)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISON)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISCELLENEOUS LAND CASE APPLICATION NO. 125 OF 2022**
**EXAUD ELIAS MACHANGE & OTHERS……….PLAINTIFF**
**VERSUS**
**VICTOR STEVEN MANG'ANA & OTHERS….RESPONDENTS**

**TO:**
**KAM COMMERCIAL SERVICES**
**WHEREAS** the above named **APPLICANT** has/have instituted **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **30th JUNE, 2022** at **09:00hrs BEFORE HON. A MSAFIRI, JUDGE** to answer the claim: and you are directed to bring any document which you wish to rely in support of your **COUNTER AFFIDANT.**
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the **APPLICATION** will be heard and determined in your absence.
**Given under my hand and the seal of this court, this 13th day of JUNE, 2022**

DEPUTY REGISTRAR HIGH COURT LAND DIVISION

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO.125 OF 2022**
**EXAUD ELIAS MACHANGE&OTHERS…….PLAINTIFF**
**VERSUS**
**VICTOR STEVEN MANG'ANA&OTHERS….RESPONDENTS**

**TO:**
**KAM COMMERCIAL SERVICES**
**WHEREAS** the above named **PLAINTIFF** has /have instituted **PLAINT** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **30th JUNE,2022 AT 09:00 hrs BEFORE HON.A.MSAFIRI,JUDGE** to answer the claim; and you are directed to bring any document which you wish to rely in support of your defense.
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the **PLAINT** will be heard and determined in your absence
**Given under my hand and the seal of this court, this 13th day of JUNE,2022**

DEPUTY REGISTRAR HIGH COURT LAND DIVISION

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**PAUL BATHOLOMEO MALLYA** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye usajili namba **T498 AGH** yenye chassis namba **LHL140023343** na kadi nyingine yenye usajili namba **T377 ACB** yenye chassis namba **LH6LV0079182.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/241556/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KOROGWE**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBA 03/2022**
**Mombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya DANIEL RAPHAEL KAMWONGA**
**………………MAREHEMU**
**DHIDI YA**
**CATHBERT LEONARD KAMWANGA……… MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**
Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo.
Mapingamizi yote kuhusu maombi haya yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 mwezi wa 06 mwaka 2022.
**Hati hii imetolewa tarehe 13 mwezi wa 06 mwaka 2022.**

HAKIMU MKAZI KOROGWE
MAHAKAMA YA WILAYA KOROGWE

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 72 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late WILLIAM CHARLES MATONYA**

**By 1. LUCY MELKIORY KAVISHE**
**2. ……………………………………………**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 29 day of 06. 2022
Dated at **MOROGORO** this **17 day of 06…2022**

**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY HASSAN JAAFAR** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili T 823 CQD aina ya **SCANIA**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya Polisi: MBE/TUK/RB/235480/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MAKOLE**
**Kituo cha MAKOLE**
**Shauri a madai/Ndoa Na 44/2022**
**Jina la Mdai: SAIMON GERALD MANYARA**
**Jina la Mdaiwa: LINNAH JOHN KEEN**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: LINNAH JOHN KEEN**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake YA TALAKA (KUACHANA)

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katikaMahakama hii **Tarehe 06 Mwezi 07 Mwaka 2022 saa 2.30** asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022**

……………………………………
**HAKIMU**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

KWA HABARI MOTOMOTO
USIKOSE GAZETI
LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Viongozi EAC wakutana kujadili mzozo DRC

**NAIROBI,** Kenya

VIONGOZI wa mataifa saba yanayounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wanatarajiwa kukutana kujadili hali ya usalama katika eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Viongozi hao wanakutana kwa mualiko wa mwenyeji wao Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta ambaye ni mwenyekiti wa Jumuiya hiyo.

Muda mfupi uliopita Rais wa Uganda Yoweri Museveni amethibitisha kwenye mtandao wake rasmi wa Twitter kwamba aliwasili jijini Nairobi kuhudhuria kikao cha tatu cha wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Rais Kenyatta alitoa wito wa kupelekwa kwa Kikosi cha Kudumu cha Afrika Mashariki ili kukomesha ghasia katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo. DRC hata hivyo inapinga Rwanda kuwa sehemu ya jeshi lililopendekezwa la kikanda na imesitisha uhusiano wa pande mbili na Kigali.

Nchi hiyo inaishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 ambao hivi majuzi waliuteka mji wa mpakani Bunagana.

Hata hivyo, Rwanda inakanusha madai hayo. Rais Felix Tshisekedi katika taarifa yake aliishutumu Rwanda kwa kutaka kuikalia kimabavu nchi yake ili kutumia madini yake na kuitaka Uingereza kuishinikiza Kigali kukomesha uchokozi wake.

Mvutano kati ya nchi hizo mbili umeongezeka katika wiki za hivi karibuni huku maandamano ya kuipinga Rwanda yakiripotiwa mjini Kinshasa na mashariki mwa Congo.

Siku mbili zilizopita, mwanajeshi wa Congo aliwafyatulia risasi walinda usalama wa Rwanda katika kituo cha mpakani mjini Bukavu na kuwajeruhi maofisa wawili wa polisi.

Kenya ndiyo mwenyeji wa mazungumzo ya moja kwa moja ya amani kati ya serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na makundi tofauti vya waasi. **BBC**

## Jino la Lumumba lakabidhiwa kwa familia

**KINSHASA,** DRC

MAMLAKA ya Ubelgiji imekabidhi jino la mpigania uhuru wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kwa familia yake katika hafla iliyofanyika jijini Brussels.

Jino hilo ni sehemu pekee ya mabaki ya mwili wa kiongozi huyo ambaye inadhaniwa kuwa bado ipo baada ya kunyongwa na kisha mwili wake kuyeyushwa kwa tindikali mnamo 1961. Ubelgiji ilikuwa koloni la nchi hiyo na uchunguzi rasmi ulisema kwamba baadhi ya wanachama wa serikali yake wakati huo waliwajibika kimaadili kwa kifo chake.

Polisi wa Ubelgiji, Gerard Soete, aliyesimamia kuharibiwa kwa mwili huo, alichukua jino hilo kama aina ya nyara ya uwindaji. **BBC**

# Ukraine sasa yapoteza udhibiti eneo la Metolkin

**KYIV,** Ukraine

MKUU wa utawala wa kijeshi wa eneo la Luhansk, Sergei Gaidai, amesema kuwa wanajeshi wa Ukraine wamepoteza udhibiti wa kijiji cha Metelkino karibu na Severodonetsk.

"Mapigano yanaendelea katika vijiji vingi karibu na Severodonetsk na Lisichansk. Kwa bahati mbaya, kwa sasa hatudhibiti eneo la Metelkino karibu na kituo cha kikanda," Gaidai alisema.

Asubuhi ya jana, Russia ilizidisha mapigano katika eneo la viwanda la Severodonetsk na nje kidogo ya jiji hilo.

Russia inataka kupata mafanikio na mapigano yanayofanyika katika vijiji vingi karibu na Severodonetsk na Lysychansk. "tumepoteza katika vita, lakini mkoa wa Luhansk utatetewa hadi mwisho, tutazuia jeshi kwa muda mrefu iwezekanavyo," alisema Gaidai.

Kulingana na Gaidai, kazi ya uokoaji wenye utulivu inaendelea kwenye eneo la Lysychansk.

Gaidai anadai kwamba Lysychansk inateseka kutokana na kushambuliwa kwa makombora, na kwamba wasaliti wa ndani wanachochea hali hiyo.

**RUSSIA INAZUIA MASHAMBULIZI UKRAINE**

Imeelezwa Russia inatumia ndege za kivita na mizinga katika maeneo mengi ili kuzuia kusonga mbele kwa askari wa Ukraine.

**Katika eneo la Donetsk, askari wa Russia wanaendelea kuzingira eneo la Severodonetsk na Bakhmut, wakitumia ndege za kivita.**

Mashambulizi kama hayo yalifanywa na wanajeshi wa Russia huko Slobozhansky, Kharkov, Slavyansky, Donetsk, Severodonetsky, Bakhmutsky, Limansky, Avdeevsky, Kurakhovsky, Novopavlovsky na maeneo ya Zaporozhye, ripoti hiyo ilisema.

Katika eneo la Kharkiv, juhudi za wanajeshi wa Russia zinalenga kuzuia kusonga mbele kwa vikosi vya ulinzi kwenye mpaka wa jimbo la Ukraine.

Vikosi hivyo vilifyatua risasi kwa nguvu kutoka maeneo ya makazi ya Kazachya Lopan, Malye Prohody, Dementievka, Petrovka, Verkhniy Saltov, Rubizhnoye na Kharkov.

Katika eneo la Donetsk, askari wa Russia wanaendelea kuzingira eneo la Severodonetsk na Bakhmut, wakitumia ndege za kivita.

**UKRAINE YAONYA ITAZIDISHA MASHAMBULIZI**

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ameonya kwamba Russia itazidisha mashambulizi dhidi ya nchi yake katika siku zijazo, huku nchi hiyo ikisubiri jibu kuhusu azma yake ya kujiunga na Muungano wa Ulaya (EU).

Wanachama wa Muungano huo wanatarajiwa kuamua ikiwa watatoa hadhi ya mgombea Kyiv baadaye wiki hii.

Hatua hiyo itaanzisha mchakato wa Ukraine kujiunga na muungano huo, ambao unaweza kuchukua miaka kadhaa kukamilika.

Lakini Zelensky alionya uamuzi huo unaweza kuifanya Russia kuongeza mashambulizi yake.

Akizungumza wakati wa hotuba yake ya usiku kutoka Kyiv, kiongozi huyo alisema yeye na washauri wake wanatarajia shughuli kubwa zaidi kutoka kwa adui, lakini aliwaambia raia kwamba vikosi vyake vinajiandaa na viko tayari kwa mashambulizi yoyote mapya.

Aliahidi kuendelea mbele kile alichokiita matarajio ya kihistoria ya Ukraine kujiunga na EU, ambayo yaliidhinishwa na watendaji wakuu wa umoja huo na Tume ya Ulaya, wiki iliyopita.

Uamuzi huo kwa sasa uko mikononi mwa Baraza la Ulaya, chombo kilichoundwa na viongozi wa nchi wanachama, ambacho kitakutana katika mkutano wa kilele huko Brussels Alhamisi na Ijumaa. **BBC**



Sara Duterte akila kiapo akiwa amesimama kando ya wazazi wake, akiwamo baba yake Rais Rodrigo Duterte. **PICHA: BBC**

# Sara Duterte aapa kuwa makamu wa rais

**MANILA,** Ufilipino

SARA Duterte ambaye ni binti wa Rais wa Ufilipino ambaye anamaliza muda wake, ameapishwa kuwa makamu wa rais wa nchi hiyo.

Kiongozi hiyo amesema atawaunganisha Wafilipino katika hafla ya kuapishwa kwake mjini Davao.

Shughuli hiyo ilifanyika katika mji ambao Sara mwenye umri wa miaka 44, alichukua usukani kutoka kwa baba yake kama Meya kwa zaidi ya mwongo mmoja uliopita.

Alikula kiapo kando ya mgombea mwenzake, Ferdinand Marcos Junior, ambaye hivi karibuni atachukua nafasi ya baba yake kama rais.

"Siku zinazokuja zinatarajiwa kuwa na changamoto ambazo zinatuhitaji kuwa na mshikamano kama taifa," alisema Duterte Muhula wake wa miaka sita madarakani ukiongozwa na Ferdinand Marcos Junior, utaanza rasmi Juni 30.

Kama wangombea katika uchaguzi wa mwezi Mei, wawili hao walipata ushindi wa kishindo kwa kubuni muungano thabiti wa kisiasa na kutumia kauli mbiu ya umoja ambao utasaidia baadhi ya washirika wao pia kupata uongozi katika ngazi zingine za serikali.

Nchini Ufilipino, rais na makamu wake wanachaguliwa pamoja.

Rais Duterte ni mtu mwenye utata ambaye aliingia madarakani mwaka 2016 akiahidi kupunguza uhalifu na kukabiliana na janga la dawa za kulevya. **BBC**

HABARI MICHEZO

# MATOLA AFUNGUKA USHINDI SIMBA IKIFANYA YAKE TENA

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, amesema walistahili kupata ushindi dhidi ya KMC FC kutokana na kiwango kikubwa kulichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi.

**Katika mechi hiyo, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-1, huo ukiwa ni ushindi wa pili mfululizo kwa Matola, tangu aanze kuiongoza timu hiyo baada ya kuondoka Kocha Mkuu, Mhispania Pablo Franco.**

Mchezo wa kwanza Simba chini ya Matola, iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mbeya City uwanjani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola alisema walicheza vizuri muda wote, na wachezaji walijitahidi kufuata maelekezo aliyowapa katika uwanja wa mazoezi licha ya kipindi cha kwanza kufanya makosa na kutoa nafasi kwa wapinzani kupata bao la mapema.

Alisema kipindi cha kwanza KMC walingia kwa njia ya kuzuia, wote wakawa nyuma ya mpira, lakini waliwafungua na kuweza kuwafunga katika mchezo huo.

"Ukiangalia mchezo mzima tulikuwa bora zaidi yao, tulitengeneza nafasi nyingi na tulistahili kupata ushindi kwa kuwa tulicheza vizuri," alisema na kuongeza;

"KMC FC walitusumbua kipindi cha kwanza kwa kuwa wote walikuwa nyuma walikuwa wanazuia tu, lakini tulivyorudi kipindi cha pili tulitafuta njia za kuwafungua na kufanikiwa kupata mabao yote matatu," alisema Matola.

Alisema KMC FC walimilika safu ya kiungo hali iliyomfanya kufanya mabadiliko katika kikosi chake kwa kumpunguza kiungo na kuongeza mshambuliaji jambo lililofanikisha kupata ushindi huo.

Wakati huo huo aliyekuwa kiungo wa Simba, Larry Bwalya ambaye ameuzwa hivi karibuni aliwaaga mashabiki wa timu hiyo na kuwashukuru wachezaji na benchi la ufundi kwa ushirikiano mkubwa waliompa katika kipindi chote alichokuwa klabuni hapo.

Alisema anaweza kurudi kama Mungu atamjalia kwa kuwa kazi ya soka ni mzunguko wa kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Nawashukuru sana mashabiki kwa upendo mkubwa walionionyesha, wamenipa thamani kubwa na najiona mwenye bahati kuwa na familia hii, siku zote Simba itabaki kuwa moyoni mwangu," alisema Bwalya.

Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema walizidiwa na wapinzani wao, Simba walikuwa bora katika mchezo huo licha ya wao kufanikiwa kupata bao la kwanza na kushindwa kulilinda.

"Simba walikuwa bora kipindi cha pili kiufundi na kimbinu katika mchezo huo, tulifanya makosa na kushindwa kulilinda bao letu tulilopata kipindi cha kwanza," alisema Ahmad.



Pape Sakho akishangilia na kupongezwa na mchezaji mwenza wa Simba, Israel Mwenda baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikishinda 3-0 dhidi ya KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**

# *Lule: Ruvu wamejimaliza wenyewe*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule amesema wapinzani wao, Ruvu Shooting walijimaliza wenyewe kutokana na viungo wao kushindwa kukaba, hivyo kuwapa nafasi viungo wa timu yake kutawala dimba na kufanya wanavyotaka.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hizo, ambayo Mbeya City ilishinda bao 1-0 ugenini juzi katika Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani lililowekwa wavuni na Baraka Mwalubunju, Lule alisema ushindi walioupata ni kama vile wamezawadiwa na wapinzani wao.

"Ushindi huu tumeupata kwa sababu tuliwazidi sana wenzetu, kwa jinsi mechi ilivyokuwa inachezwa nilijua tu nitashinda kwa sababu viungo wao wa kati walikuwa hawakabi, hivyo waliwapa uhuru mkubwa viungo wangu kucheza wanavyojisikia na kuwalisha kwa urahisi washambuliaji wangu.

Kuna kijana wangu pale kati kusema kweli inabidi nimpongeze, alitawala kabisa kati pale, anaitwa Jamal Dulaz, alitumia udhaifu wao vizuri sana, alicheza akiwa huru, na tulivyokuwa tunacheza ni kwamba wakati tunajilinda tulitumia mfumo wa 4-4-1-1 na tukishambulia tunageuka na kutumia 4-4-2," Lule alitoa siri hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, alisema pamoja na kufungwa hajakata tamaa kwa sababu bado mechi mbili kabla ya kumaliza ligi, hivyo lolote linaweza kutokea.

"Tulipata nafasi kadhaa tumeshindwa kuzitumia, lakini wenzetu chache tu wametumia moja, na nisema tu wakati mwingine kwenye soka kuna kitu kama bahati, lakini ligi bado, tuna mechi mbili lolote linaweza kutokea, tutajipanga," alisema.

Hayo ni matokeo ambayo yanaifanya Mbeya City kushika nafasi ya saba kwa pointi 35, huku Ruvu Shooting ikiwa nafasi ya 13 na pointi 28.

# Tanzania yatwaa ubingwa Kriketi

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Kriketi, imetwaa ubingwa wa mashindano ya Kwibuka Tournament 2022, yaliyomalizika nchini Rwanda juzi.

Mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka ni kwa ajili ya kukumbuka mauaji ya kimbari yaliyofanyika nchini humo mwaka 1994.

Mashindano hayo yalianza Juni 9 hadi 18, mwaka huu na kushirikisha nchi nane ikiwamo Tanzania ambayo imetwaa ubingwa huo kwa mara ya pili baada ya kuubeba mwaka 2019 kwa mara ya kwanza.

Nchi zingine zilizoshiriki ni Kenya, Botswana, Ujerumani, Brazil, Nigeria, Uganda na wenyeji wa michuano hiyo, Rwanda.

Tanzania imetwaa ubingwa huo baada ya kuishinda Kenya kwa mikimbio 60 katika mchezo wa fainali.

Mbali na kuibuka na ubingwa huo, pia Tanzania imeng'ara katika mashindano ya mchezaji mmoja mmoja kwa kuondoka na tuzo ikiwamo ya mchezaji bora wa fainali iliyoenda kwa Perice Zakaya.

Nasra Nasoro na Mwanaidi Ammy kutoka timu ya Tanzania pia wameondoka na tuzo ya wachezaji bora wa mashindano hayo kwa ujumla wakati Nasra na Fatuma Kibasu walijumuishwa kwenye timu ya waliofanya vema katika, lakini Kibasu akichaguliwa katika kikosi bora cha mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Chama cha Mchezo wa Kriketi (TCA), Atif Salim, alisema timu hiyo ilirejea jana baada ya kufanya vizuri katika mashindano hayo.

"Huu ni ubingwa wetu wa pili kwa sasa, mwaka 2019 tulifanikiwa kutwaa taji hili na sasa, lakini tumefanya vizuri kwa kuondoka na tuzo kadhaa ikiwamo mchezaji bora wa fainali na mashindano," alisema Atif.



## ZISIKUPITE

### SPURS KUIPIKU ARSENAL

KLABU ya Tottenham Hotspur ina matumaini ya kuwapiku mahasimu wao wa Kaskazini mwa London, Arsenal katika mbio za kumsaka mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus. ***(Mirror)***

### STERLING ANUKIA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akiwauliza watu kuhusu maisha kule Magharibi mwa London huku klabu ya Chelsea ikiwa na nia naye. ***(Athletic)***

### AKE ATAKIWA STAMFORD

KLABU ya Chelsea inaweza pia kumhitaji mlinzi wa Manchester City mwenye umri wa miaka 27, Nathan Ake. ***(Telegraph)***

### LUKAKU KUREJEA INTER

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kurejea Inter Milan kwa gharama ya mkopo wa pauni milioni 8.5 pamoja na marupurupu yatakayokubaliwa baina ya klabu hizo. ***(Mail)***

### UNITED NA DE JONG

KLABU ya Manchester United inaangalia uwezekano wa kutoa ofa nyingine kwa ajili ya kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, Frenkie de Jong. ***(Fabrizio Romano)***

### NEVES KUNG'OLEWA WOLVES

KIUNGO wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, yuko katika orodha ya Manchester United ya wachezaji inayoweza kuwajali iwapo watashindwa kumsainisha Frenkie de Jong. ***(Fabrizio Romano, via givemesport)***

### NEWCASTLE YAITIWA BAILLY

KLABU ya Newcastle United imepewa ofa ya kumsajili, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 28, kutoka Manchester United. ***(Mirror)***

### DAU LA DIABY LATAJWA

NEWCATLE United pia wameambiwa kuwa ni lazima walipe pauni milioni 50 ili kumsajili winga wa Bayer Leverkusen na Ufaransa, Moussa Diaby. ***(Sun)***

### RONALDO AAFIKI YA UTD

NYOTA WA Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, ameafiki hoja ya Manchester United ya kusaini mkataba na mshambuliaji mpya. ***(Express)***

### GAAL KAHUSIKA KWA TIMBER

KOCHA wa Uholanzi, Louis van Gaal alihusika kwa sehemu kubwa katika kumzuia mlinzi wa Ajax, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 21 kuhamia Manchester United. ***(Marcel van der Kraan, Sky Sports)***

### RUDONI LULU ENGLAND

KLABU za Sunderland, Huddersfield na Bristol City, zimeweka dau la nyongeza la pauni milioni moja kwa ajili ya kiungo wa kati mwenye umri wa miaka 21, anayeichezea klabu ya AFC Wimbledon, Jack Rudoni. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AANIKA ALIVYOTAKA KUSTAAFU KUKIPIGA UFARANSA

**Tulikutana kwa dakika tano ofisini kwangu, alikuwa na hasira, hakutaka kuichezea tena...**

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema alikaribia kustaafu kuichezea Ufaransa kutokana na kukosolewa kwa kiwango chake kwenye michuano ya Euro 2020, akifichua kuwa ubaguzi wa rangi ndio ambao ulimfanya akaribie kustaafu kutoka 'Les Bleus'.

**Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, Noel Le Graet aliiambia Le Journal du Dimanche kwamba, Mbappe alikuwa na hasira na hakutaka kuichezea nchi yake tena baada ya kukabiliwa na mashabiki wenye hasira.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alishindwa kufunga bao katika mechi zake nne mwaka jana, na Ufaransa ilitolewa na Uswisi katika hatua ya 16-bora.

Mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain, Mbappe alikosa mkwaju wa penalti huku mabingwa hao watetezi wa dunia wakipokea kichapo cha kushtukiza kwa mikwaju ya penalti. Mbappe alijibu maoni ya Le Graet kupitia Twitter: "Ndiyo, hata hivyo, nilimweleza waziwazi kwamba ilikuwa kuhusiana na ubaguzi wa rangi na si kwa adhabu."

Kama kiongozi mchanga wa timu ya Ufaransa, Mbappe alikabiliwa na ukosoaji mkali alipokuwa akijitahidi kuleta matokeo kwenye mashindano.

Le Graet alisema katika mahojiano na gazeti la Jumapili: "Nilikutana naye baada ya Euro. Alihisi kuwa shirikisho halikumtetea baada ya kukosa penalti na ukosoaji aliokumbana nao kwenye mitandao.

"Tulikutana kwa dakika tano ofisini kwangu. Alikuwa na hasira, hakutaka kuichezea timu ya Ufaransa tena - jambo ambalo bila shaka hakumaanisha.

"Unajua jinsi ilivyo; yeye ni mshindi, alichanganyikiwa sana, kama sisi sote, kwa kuondolewa. Yeye ni rafiki wa vyombo vya habari. Yeye ni mtu mzuri."

Mbappe ameendelea kuichezea Ufaransa mara tisa zaidi tangu mwaka jana kwenye michuano ya Euro 2020, na kuisaidia nchi yake kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar. Amefunga mabao 27 katika mechi 57 za wakubwa kwa nchi yake.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 260,
MECHI KALI
VIDAR
VERSUS
BRYNE
1 | 6.30
X | 4.43
2 | 1.40
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ BADO MUHIMU INTER




**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez bado ni "muhimu" kwa Inter Milan, wakati 'Nerazzurri' hao pia wakiendelea na mazungumzo na Romelu Lukaku ili kuona kama kuna nafasi ya kufanya makubaliano.

Huo ni ujumbe kutoka kwa mkuu wa Inter, Giuseppe Marotta, ambaye jana, Jumatatu alizungumza na Radio Anch'Io ili kutoa taarifa kuhusu biashara yao ya uhamisho.

Inasemekana Lukaku atarejea Inter kwa mkopo chini ya mwaka mmoja baada ya kuondoka Italia na kusajiliwa tena Chelsea kwa uhamisho uliovunja rekodi ya klabu kwa pauni milioni 97.5, akiwa amefunga mabao nane pekee katika mechi 26 za Ligi Kuu England.

Mshambuliaji huyo aliiwezesha Inter Milan kushinda Scudetto msimu wa 2020-21 na katika kipindi chake cha miaka miwili, hakuna mchezaji wa Nerazzurri aliyefunga mabao zaidi (64), alitoa pasi za mabao zaidi (17) au kutengeneza nafasi nyingi (133) katika mashindano yote.

Paulo Dybala pia anaonekana kujiunga na Inter kwa uhamisho huru kutoka Juventus huku mazungumzo ya uhakika ya Marotta yakiendelea kuwaleta washambuliaji hao kwenye kikosi cha Simone Inzaghi.

"Ni vigumu kutoa jibu sahihi. Hayo ndio malengo yetu, lakini lazima tutathmini fedha," alisema, kama alivyonukuliwa na FCInternews.

"Siwezi kuficha kuwa tunawataka wachezaji hawa, tunataka kuwasajili. Ikiwa sivyo, tutaendelea na malengo mengine.




# Donnarumma: Natamani sana kubeba taji la Uefa

**ROME,** Italia

GOLIKIPA Donnarumma amesema licha ya klabu yake ya Paris Saint-Germain kushinda taji la Ligue 1, lakini anajua hawawezi "kuridhika kikamilifu" kwa sababu ya kushindwa kubeba Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Donnarumma alisajiliwa na PSG kabla ya msimu wa 2021-22, huku Achraf Hakimi, Sergio Ramos, Georginio Wijnaldum na Lionel Messi pia wakiwasili katika mji huo mkuu wa Ufaransa.

Messi aliungana na Kylian Mbappe na Neymar kuunda safu ya mbele ya kutisha, huku PSG ikijiweka sawa na kutwaa taji la 10 la Ligue 1 lililoongeza rekodi, likiwa ni la nane katika misimu 10 iliyopita.

Ushindi huo wa ubingwa pia ulikuwa taji la kwanza la Mauricio Pochettino kama kocha, lakini bosi huyo wa zamani wa Tottenham anaonekana kuelekea kwenye mlango wa kutokea baada ya kushindwa kuleta mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mbappe alifunga katika mechi zote mbili za hatua ya 16-bora dhidi ya Real Madrid, lakini hat-trick ya ajabu ya Karim Benzema ilichochea mabadiliko kwa 'Los Blancos', ambao walichukua ubingwa Mei.

## HABARI MICHEZO


,838,830

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 .21/06/22 | 22:30 | Levadia Tallinn vs Vikingur Reykjavik | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02 .22/06/22 | 01:00 | Aldosivi vs CA Platense | 2.74 | 2.99 | 2.50 |
| 03 .22/06/22 | 03:30 | Central Cordoba vs San Lorenzo | 2.33 | 3.00 | 2.95 |
| 04 .22/06/22 | 13:00 | Gamba Osaka vs Oita Trinita | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 05 .22/06/22 | 13:30 | Bucheon vs Anyang | 2.41 | 3.10 | 2.76 |
| 06 .22/06/22 | 18:00 | Seinajoen JK vs Haka | 2.44 | 3.05 | 2.76 |
| 07 .22/06/22 | 18:30 | Japs vs MP Mikkeli | 2.24 | 3.30 | 2.86 |
| 08 .23/06/22 | 00:00 | Resistencia FC vs 12 de Octubre de Itaugua | 2.38 | 2.99 | 2.89 |
| 09 .23/06/22 | 01:30 | Bahia BA vs Atletico Pr | 2.62 | 2.91 | 2.67 |
| 10 .23/06/22 | 02:00 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.31 | 3.00 | 3.00 |
| 11 .23/06/22 | 03:00 | NY Red Bulls vs New York City | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 12 .24/06/22 | 02:00 | Sao Paulo vs Palmeiras | 2.70 | 3.04 | 2.50 |
| 13 .24/06/22 | 03:30 | CSA AL vs Gremio | 3.15 | 2.85 | 2.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 21/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1305 | Sheikh Russel KC vs Sheikh Jamal | 3.24 | 3.34 | 2.03 |
| 13:00 | 2036 | Sangju Sangmu vs Seongnam Ilhwa | 1.78 | 3.39 | 4.13 |
| 13:00 | 3314 | Rahmatgonj Mfs vs Bashundhara Kings | 12.75 | 6.67 | 1.15 |
| 13:00 | 4779 | Daejeon Citizen vs Gwangju | 2.66 | 3.20 | 2.43 |
| 13:00 | 5078 | Abahani Ltd. Chittagong vs Saif SC | 2.76 | 3.16 | 2.38 |
| 13:30 | 3881 | Gimpo Citizen vs Jeonnam Dragons | 2.60 | 3.09 | 2.55 |
| 13:30 | 5223 | Suwon City vs Pohang Steelers | 3.38 | 3.43 | 1.95 |
| 13:30 | 5381 | Daegu vs Jeju Utd | 2.75 | 3.09 | 2.42 |
| 14:30 | 4413 | Beijing BG vs Shenyang City FC | 3.29 | 3.04 | 2.14 |
| 14:45 | 3852 | Geylang Int. vs Young Lions | 1.76 | 4.03 | 3.54 |
| 15:00 | 1462 | Shandong Luneng vs Dalian Aerbing | 1.34 | 4.52 | 7.66 |
| 16:00 | 5318 | La Fiorita vs Inter Club De Escaldes | 5.80 | 3.50 | 1.61 |
| 17:00 | 1323 | Merani Martvili vs Shukura | 2.31 | 3.24 | 2.80 |
| 17:00 | 2714 | Gareji vs FC Samtredia | 2.37 | 2.74 | 3.19 |
| 18:00 | 1093 | BFC Daugavpils vs SK Super Nova | 1.68 | 3.58 | 4.41 |
| 18:00 | 2691 | Hodd 2 vs Raufoss IL 2 | 1.80 | 4.03 | 3.39 |
| 18:00 | 3667 | FC Hegelmann Litauen Kaunas vs Suduva | 2.65 | 2.84 | 2.70 |
| 18:00 | 4155 | Navbahor Namangan vs Metallurg Bekabad | 1.51 | 3.64 | 6.09 |
| 18:00 | 4903 | Bunyodkor vs Kokand 1912 | 1.77 | 3.63 | 3.87 |
| 18:30 | 1048 | Slovakia U19 vs Italy U19 | 8.87 | 5.32 | 1.25 |
| 18:30 | 4714 | FC Vaajakoski vs Vifk Vaasa | 2.14 | 3.55 | 2.86 |
| 18:30 | 5441 | HJS Akatemia vs Tampere United | 2.54 | 3.81 | 2.25 |
| 19:00 | 1440 | Saburtalo Tbilisi vs FC Telavi | 2.33 | 2.98 | 2.98 |
| 19:00 | 3003 | Atlantis FC vs Keski Uusimaa | 1.95 | 3.78 | 3.09 |
| 19:00 | 3198 | Spartaks Jurmala vs FS Metta/Lu | 2.38 | 3.04 | 2.84 |
| 19:00 | 3562 | Vidar vs Bryne | 6.30 | 4.43 | 1.40 |
| 20:00 | 3185 | Banga Gargzdai vs Vilniaus Riteriai | 4.32 | 3.09 | 1.84 |
| 20:00 | 3796 | Zenit St Petersburg vs Nizhny Novgorod | 1.34 | 4.72 | 7.09 |
| 21:00 | 1053 | Vidir vs DalvikÂk/Reynir | 2.02 | 3.68 | 2.99 |
| 21:00 | 5665 | Romania U19 vs France U19 | 9.63 | 5.50 | 1.23 |
| 21:30 | 3831 | East Fife vs Civil Service United | 1.60 | 4.20 | 4.60 |
| 21:30 | 4736 | Alloa Athletic vs Partick Thisle | 3.10 | 3.65 | 2.07 |
| 21:45 | 3078 | The New Saints vs Bala Town | 1.56 | 4.11 | 4.60 |
| 22:15 | 1582 | IA Akranes vs Hafnarfjordur | 3.43 | 3.87 | 1.82 |
| 22:15 | 5480 | Valur vs Leiknir | 1.38 | 4.61 | 6.27 |
| 22:30 | 1469 | Levadia Tallinn vs Vikingur Reykjavik | 2.80 | 3.35 | 2.36 |

JUMATANO - 22/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 4324 | Aldosivi vs CA Platense | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 01:00 | 5182 | Chapecoense vs CRB AL | 2.14 | 2.89 | 3.48 |
| 05:30 | 3785 | LA Galaxy vs Sacramento Republic | 1.50 | 4.22 | 5.10 |
| 12:00 | 1593 | Valentine FC vs Lambton Jaffas | 6.08 | 4.71 | 1.38 |
| 12:00 | 3715 | Consadole Sapporo vs Ventforet Kofu | 2.03 | 3.20 | 3.40 |
| 12:30 | 5088 | Avispa Fukuoka vs Grulla Morioka | 1.64 | 3.54 | 4.81 |
| 13:00 | 1171 | Yokohama F Marinos vs Tochigi SC | 1.39 | 4.53 | 6.30 |
| 13:00 | 1322 | FC Tokyo vs V Varen Nagasaki | 1.89 | 3.24 | 3.83 |
| 13:00 | 2767 | Vissel Kobe vs Renofa Yamaguchi | 1.80 | 3.25 | 4.23 |
| 13:00 | 3279 | Kashiwa Reysol vs Tokushima Vortis | 1.96 | 3.15 | 3.69 |
| 13:00 | 3458 | Mohammedan Sporting Club Dhaka vs Dhaka Abahani | 4.62 | 3.74 | 1.62 |
| 13:00 | 3472 | Gyeongnam vs Chungnam Asan | 2.19 | 3.24 | 2.99 |
| 13:00 | 3633 | Urawa Red Diamonds vs Thespakusatsu | 1.70 | 3.43 | 4.51 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KMKM YAKABIDHIWA 'NDOO' YA UBINGWA LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mabaharia wa KMKM wamekabidhiwa rasmi Kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu wa 2021/2022 hapo katika mchezo wa mwisho wa ligi hiyo uliochezwa Uwanja wa Amaan juzi.

**Katika mchezo huo, KMKM walipokea kombe hilo kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mlandege.**

Mbali na kombe hilo, pia KMKM wamekabidhiwa hundi ya shilingi milioni 30 kutoka kwa Mdhamini Mkuu, Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kukabidhiwa kombe hilo, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema ametimiza lengo lake la kuutetea ubingwa wao kwa mara nyingine msimu huu.

Alisema ulikuwa msimu mzuri kwa upande wao kwa kufanikisha jambo lao la ubingwa licha ya kwamba ulikuwa msimu mgumu kutokana na ushindani mkubwa ulionyeshwa na klabu zote.

"Tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufanikisha jambo letu hili la kuchukua ubingwa, lakini shukrani pekee kwa wachezaji na benchi la ufundi kwa pamoja hakika sote tumefanikisha," alisema.

Aidha, ameipongeza Bodi ya Ligi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka visiwani hapo (ZFF), kwa kuhakikisha msimu huu ligi imechezwa kama ilivyopangwa kwa mujibu wa ratiba bila kukwama licha ya changamoto kadhaa ambazo kibinadamu hazikuweza kuepukika.

Hata hivyo, alisema wanajiandaa kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu wa 2021/22, KMKM wakiwa na viongozi wa timu hiyo baada ya kukabidhiwa kombe juzi. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# *Staa Simba aponda mastraika Bongo*

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa Simba, Malota Soma 'Ball Juggle', amesema mastraika wa sasa nchini hawana wivu wa maendeleo, hawajitumi, wavivu na wamekosa ubunifu ndiyo maana hawafungi mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine, tofauti na wale wakigeni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Malota aliyeichezea Simba miaka ya 1980 hadi 1990 mwanzoni, alisema kinachowagharimu mastraika wa sasa hawataki kuiga mazuri kutoka kwa wachezaji wenzao ambao wamefanikiwa kisoka.

"Mpira ni ule ule tu wa zamani na sasa, huko nyuma wachezaji walikuwa wanajitambua, walicheza kwa kutafuta sifa mitaani na popote watakapopita, pamoja na kuzisaidia timu zao, kwa hiyo kila mmoja alikuwa anaangalia udhaifu wake kama ni kufunga, kupiga mashuti, kukokota mpira, basi walifanya wenyewe mazoezi ya ziada bila kocha ili kufanyia kazi udhaifu wake.

"Kingine ninachowagharimu vijana wa sasa ni kwamba hawana wivu wa maendeleo ya kutaka kuwa kama fulani, au mfungaji fulani, siyo vibaya kuiga na kama huigi mchezaji yeyote huwezi kuwa mchezaji mzuri," alisema mchezaji huyo ambaye mara nyingi alikuwa akicheza kama msaidizi wa straika, namba kumi.

Aidha, alishangaa kuona kwa sasa sheria zimerekebishwa sana na kutoa uhuru mno kwa mastraika, lakini bado wamekuwa waoga na kutojiamini.

"Zamani kulikuwa na mabeki kama Daud Salum 'Bruce Lee', Mohamed Kajole wa Simba, Boi Wickens na Salum Kabunda Ninja wa Yanga na wengine wengi, walikuwa mabeki katili sana, wanaweza kukufanya chochote, anaweza kukurukia hata miguu miwili na isiwe faulo, bado kuna watu walikuwa wanafunga mabao, lakini sasa sheria zimebadilika sana, faulo hiyo ni kadi nyekundu, lakini naona bado hawafanyi vizuri, sasa wangekutana na wale jamaa ambao hacheki mtu mpaka mpira unaisha ingekuwaje?" Akahoji mchezaji huyo aliyesifika kwa chenga za maudhi na nguvu enzi zake.

Aliwataja mabeki ambao angalau wanaonekana kama wale wa zamani na anaowakubali ni Kelvin Yondani, Juma Nyosso, Agrrey Morris na Joash Onyango.

# Michezo

Jumanne Juni 21, 2022

Nipashe




Mbappe aanika alivyotaka kustaafu UKURASA 21

KWAHERI...




Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, akimpa mkono wa kwaheri sambamba na kumkabidhi jezi ya shukrani, kiungo wa timu hiyo, Rally Bwalya, kabla ya kuichezea timu hiyo mechi ya mwisho juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya KMC FC. Simba ilitumia mchezo huo wa Ligi Kuu kumuaga Bwalya ambaye imemuuza katika Klabu ya Amazulu ya Afrika Kusini. **PICHA: SIMBA**

## Martinez bado muhimu Inter Milan

**MILAN,** Italia

AUTARO Martinez bado ni "muhimu" kwa Inter Milan, wakati 'Nerazzurri' hao pia wakiendelea na mazungumzo na Romelu Lukaku ili kuona kama kuna nafasi ya kufanya makubaliano.




HABARI UK. 22



HABARI UK. 23

## Mastraika Bongo wapondwa ubora

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa Simba, Malota Soma 'Ball Juggle', amesema mastraika wa sasa nchini hawana wivu wa maendeleo, hawajitumi, wavivu na wamekosa ubunifu ndiyo...

# SIMBA NA USAJILI WA FOWADI YA MABAO 47

## ●●● Mashine nyingine kuendelea kushushwa, yawatoa hofu mashabiki kuondoka Bwalya...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza mataji yake yote matatu msimu huu, huku chanzo kikuu kikiwa ni kukosa makali katika safu yake ya ushambuliaji, Klabu ya Simba, sasa imeonyesha imedhamiria kwa dhati kufuta kabisa tatizo hilo ili kuweza kutetea makombe yake msimu ujao na kufanya vizuri zaidi kwenye michuano ya kimataifa.

**Simba ilikaribisha msimu huu wa 2021/22 kwa kuanza kupoteza Ngao ya Jamii dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga na sasa imeupoteza ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA.**

Lakini ilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa na kuangukia Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo huko pia iliishia robo fainali kwa kutolewa na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Moja kati ya tatizo kubwa lililokuwa likilalamikiwa na Kocha Mkuu aliyetimuliwa hivi karibuni, Mhispania Pablo Franco, ni safu ya ushambuliaji kushindwa kugeuza pasi za mwisho kuwa mabao.

Pamoja na safu ya ushambuliaji ya Simba kuandamwa na majeraha ya mara kwa mara, lakini walikosa makali ya msimu uliopita wakati wote watatu, John Bocco, Chris Mugalu na Meddie Kagere walipoongozana kwenye mbio za ufungaji msimu wa 2020/21.

Hata hivyo, katika kuhakikisha wanafuta tatizo hilo, Simba imeelekeza nguvu kubwa kwenye kuimarisha safu ya ushambuliaji na tayari imeelezwa kukamilisha usajili wa washambuliaji watatu ambao mabao yao waliyofunga msimu huu jumla ni 47.

Kwanza imemalizana na kumtangaza rasmi straika Mzambia Moses Phiri kutoka Zesco ya Zambia ambaye msimu huu amemaliza Ligi Kuu ya kwao akiwa mfungaji bora namba mbili baada ya kufumania nyavu mara 14.

Kama hiyo haitoshi, taarifa za uhakika kutoka vyanzo vyetu ndani ya klabu hiyo, zimelieleza gazeti hili kuwa Wekundu wa Msimbazi hao, wamemalizana na mshambuliaji wa Vipers SC ya Uganda, Cesar Lobi Manzoki.

Manzoki mwenye uraia wa DR Congo na Jamhuri ya Afrika ya Kati, ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu Uganda msimu huu akiwa na mabao 19.

Lakini amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Msimu, Mchezaji Bora wa Wachezaji, Mfungaji Bora wa Msimu huku akiingia katika Kikosi Bora cha Msimu wa Ligi Kuu Uganda.

Nyota mwingine ambaye chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo kimeeleza Simba imemalizana naye na kilichobaki ni kumtambulisha tu ni kiungo mshambuliaji wa Bechem United ya Ghana, Augustine Okrah.

Okrah ambaye anaelezwa kuwa mnyumbulifu hatari katika nafasi yake hiyo, amemaliza msimu wa Ligi Kuu Ghana akiwa mfungaji bora namba mbili baada ya kucheka na nyavu mara 14, mabao hayo yakitokana na mechi 31 alizocheza huku pia akitoa pasi za mwisho (assists) saba.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, alipoulizwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati wakimuaga kiungo Rally Bwalya, ambaye wamemuuza katika klabu ya Amazulu ya Afrika Kusini, na wanatarajia kusajili mchezaji wa aina gani kuziba nafasi hiyo, alisema watashusha 'mashine' kali zaidi.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez wiki iliyopita, alisema bado wanaendelea kufanya mazungumzo na baadhi ya wachezaji, na mchakato huo utakapokamilika watawatangaza kupitia mitandao yao ya kijamii kama ambavyo wamekuwa wakifanya.

9 770856 541002 >